**Watu** saba wahofiwa kufia ndani ya mgodi
UKURASA 3



**Adaiwa** kumuua nduguye kisa kuku kuingia shambani
UKURASA 3


# Nipashe

Jumamosi Januari 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580469

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Bayern wamfungia kazi Upamecano**
UKURASA 20

# Waziri ageuka mbogo sakata la wajawazito

• **Ahoji** kwa nini walazwe juu ya meza, wataalamu wa afya wazuru kijijini kujiridhisha ripoti ya Nipashe... *Endelea ukurasa 2*

## yAliy OmO

uku RASA WA 5

### WATAkA Jpm ASipOkee RipOTi ku HuSu ARdHi

WANANCHI wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wamemwomba...

uku RASA WA 5

### mJAne Aliye TApeli WA AJenge WA nyumb A

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa, imemwezesha...

## kinara kidato cha nne apokewa kifalme

UKURASA 4





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Miriam Titus Msagati na bibi yake Eonica Hiza (kulia), baada ya kumkabidhi nyumba **(Picha ndogo)**, aliyoshiriki kuchangia ujenzi wake, katika Kitongoji cha Fune, Kata ya Mombo, wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. Nyumba hiyo pamoja na samani zilizomo ndani imegharimu Sh. milioni 47.32. **Habari zaidi Uk. 3. PICHA: OWM**



## Jafo atoa tamko malipo ya walimu

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**miCHezO** SimbA, mAzembe kupim AnA ubAvu UK.24

**mAOni, kATuni** UK.6

# Waziri atoa tamko wajawazito kulazwa kwenye meza kliniki

**Na Dinna Maningo,** TARIME

SIKU moja baada ya Nipashe kuripoti kuhusu watoto kupimwa uzito chini ya mti na wajawazito kupimiwa juu ya meza, kutokana na kukosa huduma ya zahanati kijijini Nyagisya, Kata ya Kiore wilayani Tarime mkoani Mara, wataalamu wa afya wamefika katika kijiji hicho kuchukua hatua.

Vilevile, serikali kupitia wizara yenye dhamana ya afya, imetoa tamko kuhusu suala hilo, akiahidi kuchukua hatua dhidi ya wahusika.

Baada ya kufika kijijini huko jana, wataalamu hao walipiga marufuku upimaji huo uliokuwa ukifanyika chini ya mti na kuagiza chumba kimoja cha ofisi ya kijiji kufanyiwa ukarabati, ili kitumike kutoa huduma za afya.

Viongozi waliofika kijijini huko jana ni pamoja na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Sylvanus Gwiboha, Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Amos Manya, Daktari Joshua Karaba kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu na Mhandisi Ujenzi, Ernest Maungo.

Wengine ni Mganga Mkuu wa Zahanati ya Kata ya Mtana, Seif Athuman, pamoja na Leonard Nyakanga ambaye ni Katibu wa Mbunge wa Tarime Vijijini.

Viongozi hao walifanya kikao na uongozi wa serikali ya kijiji na Diwani wa Kiore, Rhobi John, kujadili juu ya huduma ya kliniki inayotolewa chini ya mti na wajawazito kupimwa juu ya meza.

Baada ya kikao hicho, wataalamu hao waliwahoji wananchi ili kupata ukweli wa yale yaliyoripotiwa na Nipashe, kisha wakatembelea ujenzi wa zahanati kwa ajili ya kijiji hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Gwiboha, alisema wamepiga marufuku huduma kutolewa chini ya mti kwa kuwa ni kinyume cha mwongozo wa serikali.

Alisema huduma hiyo inatakiwa kutolewa kwenye majengo ya serikali au binafsi kulingana na maandalizi ya kijiji husika.

"Ni jambo zuri kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi maana inawasaidia kupunguza umbali, lakini siyo kutoa huduma chini ya mti, isipokuwa kwenye majengo ya serikali na binafsi.

"Kama ofisi ya kijiji kulikuwa na kikao, walipaswa kuahirisha kikao ili huduma ya kliniki iendelee.

"Ukaguzi wetu ulianzia kwenye Zahanati ya Mtana, nikamuuliza Muuguzi Rebeka Samson kwanini anatoa huduma chini ya mti, akasema ofisi ya kijiji walikuwa na kikao, nikamwambia nimekuona kwenye picha gazeti la Nipashe umependeza kweli, lakini mbona hukuvaa sare za kazi? Hilo ni kosa.

"Nikamuuliza mtendaji wa kijiji, akasema yeye amehamishiwa hapo ana miezi minne na kwamba kuna chumba cha kliniki ila kimejaa mchwa na kuna wakati waliona hadi nyoka wakaona siyo salama," alisema Gwiboha.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa halmashauri itafanya ukarabati wa chumba hicho na huduma ya kliniki itaendelea kutolewa katika kijiji hicho katika ofisi ya serikali ya kijiji na hatua za ukarabati zinaendelea, akiahidi kutoa mifuko saba ya saruji.

Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyagisya ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Central, Ghati John, alikiri maofisa hao kufika kwenye kijiji chao na walifanya kikao na kuzungumza na wananchi na kisha kutembelea eneo panapojengwa zahanati.

"Walikuja kuthibitisha kama yanayofanyika ni kweli na wakahoji wananchi, wakawaeleza ukweli ndivyo ilivyo, wao walidhani picha ni za kutengeneza, lakini wameelezwa kila kitu, bahati nzuri alikuwapo mwananchi ambaye ndiye alinunua godoro la wajawazito kulalia wakati wa kliniki.

"Tukawaonyesha chumba tulichotengwa, lakini kimejaa mchwa, mmoja akatoa Sh. 10,000, kwa ajili ya kuweka kibarua afanye usafi," alisema John.

KAULI YA WIZARA

Jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa taarifa kuhusu utolewaji wa huduma za afya kwa watoto na wajawazito kijijini Nyagisya chini ya mti na ndani ya darasa.

Katika taarifa yake hiyo, waziri huyo alisema katika gazeti la Nipashe ameona picha za watoto wakipimwa uzito chini ya mti.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali iliwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye miundombinu ya kutolea huduma za afya hasa huduma ya afya ya msingi na sekta ya afya kwa ujumla wake.

"Serikali imesikitishwa na hali hiyo, hivyo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, inafuatiliaji kwa karibu kujua nini kilitokea hadi kufikia hatua hiyo.

"Badala ya kutumia majengo mengine ya serikali yaliyopo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na hatua zitachukuliwa baada ya kupata maelezo ya kina kujua nini kilitokea," alisema Dk. Gwajima katika taarifa yake ya jana.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa picha ikionyesha mandhari ya Mji Mkongwe wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakurugenzi Watendaji wa Kampuni Binafsi Tanzania, Dino Stengel, baada ya kumaliza mazungumzo yao, Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR** .

## Jafo aagiza walimu wapya walipwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ametoa wiki moja kwa halmashauri nchini ambazo hazijawapa fedha za kujikimu walimu wapya, kuhakikisha wanawalipa ndani ya muda huo.

Jafo alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipozungumzia uboreshaji wa shule za ufundi nchini.

Alisema mwishoni mwa mwaka jana, serikali iliajiri walimu 13,000 ambao walipangwa kwenye shule mbalimbali nchini na halmashauri ziliagizwa kulipa fedha za kujikimu kwa wakati pindi watakaporipoti kwenye shule walizopangwa.

Hata hivyo, alisema kuna halmashauri hadi sasa bado hazijawapa fedha hizo na kutoa siku saba kuwalipa walimu hao.

"Sitaki kuona wanafanya kazi wakiwa na msongo wa mawazo, ninatoa wiki moja kwa halmashauri ambazo hazijalipa fedha hizo," aliagiza.

Akizungumza kuhusu uboreshaji wa shule za ufundi, Waziri Jafo aliwaagiza wakuu wa mikoa tisa yenye shule za ufundi za sekondari za serikali, kuhakikisha wanakuwa walezi wa shule hizo ili zitoe vijana wenye umahiri wa kutosha na wabobezi kwenye fani mbalimbali.

Alisema serikali imetumia Sh. bilioni 16.4 kukarabati miundombinu ya shule hizo.

Alifafanua kati ya fedha hizo, Shule ya Bwiru ilipewa Sh. milioni 825, Chato Sh. bilioni 3.9, Ifunda Sh. bilioni 3.6, Iyunga Sh. bilioni 1.01, Moshi Sh. bilioni 2.1, Mtwara Sh. bilioni 1.3, Musoma Sh. bilioni 1.2, Mwadui Sh. milioni 226 na Tanga Sh. bilioni 2.1.

Waziri Jafo alisema wakuu hao wa mikoa wenye shule hizo wanapaswa kuzitembelea na kuzungumza na walimu ikiwa ni pamoja na waajiriwa wapya ili kueleza kwa mapana mikakati ya serikali ya kuinua ubora wa shule hizo.

Alisema Sh. milioni 30 zimetengwa kwa kila shule kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zote hizo za ufundi za sekondari za serikali.

"Baada ya Rais John Magufuli kutangaza na kutoa dira ya kuelekea uchumi wa viwanda mwaka 2016, Ofisi ya Rais TAMISEMI ilichukua hatua mbalimbali, ili kufanya maandalizi ya wataalamu ambao baadaye watatumika katika viwanda vinavyoendelea kujengwa nchini," alisema.

Alisema wataalamu hao watatoka katika shule hizo za sekondari za ufundi ambapo hatua zimechukuliwa ili kuimarisha utoaji wa elimu ya ufundi na kuifanya iendane na mahitaji na ushindani katika ulimwengu wa ajira ili kuongeza pato la mwananchi wa taifa kwa ujumla. Alisema ili kuhakikisha ufundishaji na ujifunzaji katika shule hizo, Novemba mwaka jana, serikali iliajiri walimu 150 wa masomo ya ufundi wa fani mbalimbali kwa wastani wa walimu 16 kila shule.

Alifafanua kuwa Bwiru (walimu 16), Chato (walimu 18), Ifunda (walimu 16), Iyunga (walimu 17), Moshi (walimu 17), Mtwara (walimu 15), Musoma (walimu 16), Mwadui (walimu 18) na Tanga (walimu 17) na tayari fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo.

Aliongeza kuwa kwa kuwa maboresho yaliyofanyika katika shule hizo ni makubwa huku akitoa wito kwa wakurugenzi watendaji wa halmashauri wenye shule hizo kuhakikisha miundombinu na vifaa vinatunzwa.

## HABARI KITAIFA

# Watu saba wahofiwa kufia mgodini

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU saba wanaodaiwa kuingia ndani ya mashimo ya mgodi wa Barrick North Mara ulioko Nyamongo wilayani Tarime mkoani Mara kwa nia ya kuiba mawe ya dhahabu, wanahofiwa kufia ndani ya mgodi huo.

Baada ya watu hao kutoonekana tangu Desemba 5, mwaka jana, bila kuwapo taarifa zozote kuhusu waliko, familia na ndugu zao wamefika Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Tarime kutoa kilio chao wakiongozana na Diwani na wenyeviti wa vijiji walivyotoka ndugu zao hao.

Wakizungumza na Nipashe nje ya ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime juzi, wakiongozana na Diwani wa Kenyamanyori, Farida Nchagwa, aliyeongozana na wenyeviti wa mitaa, alisema wananchi hao saba wanahofiwa kupoteza maisha ndani ya mgodi huo.

Wanaohofiwa kufariki dunia ni Charles Mashiku, Nyagwisi Charles, Mnanka Werema, Matiko Merenga, Isacka Kambarage na wengine wawili waliotajwa kwa jina moja moja la Mahiri na Tereni, ambao walikuwa wanajihusisha na uchimbaji mdogo wa madini.

Alisema wachimbaji hao waliondoka Kibaga Desemba 5, mwaka jana na kueleza kuwa wanasafiri na tangu wakati huo, familia zao hazina mawasiliano nao.

"Hawapatikani kwa simu, kuna mchimbaji mwenzao waliyekuwa naye kabla kuingia mgodini, alituma ujumbe kuwajulisha ndugu kwamba hao walishafariki dunia wakiwa ndani ya mashimo ya mgodi wa Barrick North Mara kwa kulipukiwa na baruti wakiwa ndani ya shimo walimokuwa wameingia bila taarifa kutaka kuiba mawe ya dhahabu.

"Tumejaribu kufuatilia huko mgodini na kwa marafiki zao wengi, wanatuambia kuwa 'ndugu zenu walishakufa ndani ya mgodi, nendeni mkafanye matanga'.

"Kutokana na hali hiyo imetulazimu kufika huku kwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime kutaka uchunguzi ufanywe ndani ya shimo linalodaiwa kufukiwa ndugu zetu na Mkuu wa Wilaya, Mtemi Msafiri, ametuambia tuwe na subira kwani kuna tume imefika hapa wilayani kufuatilia suala hili," alisema diwani huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Msafiri, hakupatikana kuzungumzia hofu hiyo, lakini Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, John Marwa, aliiambia Nipashe kuwa suala hili linachunguzwa na kwa sasa kuna tume imefika kulifuatilia.

Mgodi wa Barrick North Mara ulioko Nyamongo, una uzio uliojengwa kuzunguka mgodi huo na kuna taa, kamera na kuna ulinzi mkali muda wote.

# Waziri Mkuu achangisha Mil. 19/- kumsaidia mtoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameendesha harambee ya papo kwa papo na kuchangisha Sh. milioni 18.9 ambapo kati ya hizo, Sh. milioni 10 zimetolewa na Rais John Pombe Magufuli.

"Mheshimiwa Rais Dk. John Pombe Magufuli anafuatilia tukio hili na amesema anamchangia Miriam Sh. milioni 10, ili ziweze kumsaidia katika mtaji wa biashara na umaliziaji wa ujenzi wa vyumba vya kupangisha," alisema.

Fedha hizo zilichangishwa kwa ajili ya Miriam Msagati, binti mwenye ulemavu wa mwili ili kumsaidia kama mtaji wa biashara na uendelezaji wa ujenzi wa vyumba vya kupangisha katika nyumba ambayo alikabidhiwa jana na Waziri Mkuu.

Gharama ya ujenzi wa nyumba na samani zilizomo ndani ni Sh. milioni 47.32.

Waziri Mkuu aliendesha harambee hiyo kwenye Kitongoji cha Fune, Kata ya Mombo wilayani Korogwe baada ya kumkabidhi binti huyo nyumba aliyojengewa na wadau mbalimbali kutokana na mchango ulioasisiwa na Majaliwa mwenyewe Machi 5 mwaka jana, alipomtembelea Miriam na kumpatia mchango wa Sh. milioni tano za kuanza ujenzi wa nyumba hiyo.

Majaliwa alimsaidia Miriam baada ya kumsikia binti akimwomba amsaidie kupata makazi yeye na bibi yake kupitia kipindi cha Wape Nafasi kinachoongozwa na Tuma Dandi, Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1).

Baada ya Waziri Mkuu kukabidhi nyumba hiyo, aliwaomba wadau wamchangie Miriam fedha ili apate mtaji pamoja na umaliziaji wa vyumba vya kupangisha ili ajitegemee.

Akiwa bado anaendesha harambee hiyo, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alizungumza na wananchi hao kupitia simu aliyompigia Waziri Mkuu, ambapo alimpongeza kwa kuhakikisha Miriam anapata makazi bora.

"Nimeona kazi kubwa iliyofanyika hapo, hongereni sana Waziri Mkuu pamoja na uongozi wa Mkoa wa Tanga, nami namwongezea Sh. milioni tano afanye mtaji," alisema.

# Adaiwa kumuua mdogo wake kisa kuku kuingia shambani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, Rainary Lugome, anadaiwa kuuawa na ndugu yake, Claus Lugome, kwa tuhuma za kuku wake kuingia katika shamba la kaka yake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issa, alisema wanawashikilia wanafamilia wawili, akiwamo baba wa watoto hao, Ado Lugome na kijana anayedaiwa kuhusika na mauaji kwa ajili ya upelelezi.

"Haya mauaji ni ya ovyo, yaani kaka kamuua mdogo wake kisa na mkasa kuku wa mdogo mtu wameenda kwenye shamba la kaka mtu," alisema Kamanda Issa na kuongeza kuwa katika upelelezi uliokuwa unaendelea, wamebaini familia hizo zimekuwa zikituhumiana kwa masuala ya ushirikina. "Katika ufuatiliaji wa suala hili, tumeona wanatuhumiana kuwa mmoja anatembea na mke wake na mwingine anamtuhumu mwenzie kuwa alikuwa anamroga," alisema.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani Njombe, linawashikilia walimu wawili wa Shule ya Sekondari Mang'oto wilayani Makete, kwa tuhuma za kusababishia ujauzito mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 na kutoa.

Issa alisema wanamshikilia Mwalimu Ezekiel Thomas (36) maarufu kwa jina la Dokole, kwa kuwa na uhusiano na mwanafunzi na kumsababishia ujauzito.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**GREEN LIGHT AUCTION MART** KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **BRAC TANZANIA FINANCE LTD, MWANZA, GEITA,TARIME,TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA AMBAZO NI NYUMBA,KIWANJA IWAPO MDAIWA HATALIPA DENI NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14)KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI**

1) Jina la mdaiwa -Baraka S. Musso,dhamana -kiwanja-mahali-bugosi -tarehe ya mnada -10/2/2021
2) Jina la mdaiwa Patric m aloyce- dhamana-nyumba,mahali-msati highway,tarehe ya mnada -11/2/2021
3) Jina la mdaiwa_Joseph W. Nyaitwe,dhamana nyumba,mahali-uwanja wa ndege,tarehe ya mnada-11/2/2021
4) Jina la mdaiwa-Charles N. Mgaya,dhamana-nyumba-mahali-nyarusahi,tarehe ya mnada-10/02/2021
5) Jina la mdaiwa -Mugaya P. Kebara,dhamana -kiwanja,mahali-ronsoti,tarehe ya mnada 11/2/2021
6) Jina la mdaiwa-Shadrack M. Chacha,dhamana-boma,mahali-biambwi,tarehe ya mnada 12/2/2021
7) Jina la mdaiwa Michael S. Chubo na Mayala Micheal,dhamana- nyumba, mahali-mbugani igoma-tarehe ya mnada 26/2/2021
8) Jina la mdaiwa-Hussein R. Masiki ,dhamana -nyumba-mahali-nyambisu,tarehe ya mnada 27/02/2021
9) Jina la mdaiwa-Steven Mabuga,dhamana -nyumba-mahali- ilalilo-tarehe ya mnad 27/2/2o21
10) Jina la mdaiwa-Victor Lema -dhamana –nyumba,mahali-mkolani,tarehe ya mnada 29/2/2021
11) Jina la mdaiwa Marryan Solomon,dhamana-kiwanja,mahali-nyamazobe,tarehe ya mnada 03/02/2021
12) Jina la mdaiwa Evans Simbaya ,dhamana - nyumba-,mahali- kambarage,tarehe ya mnada 3/2/2021
13) Jina la mdaiwa Samwel Luchele ,dhamana- kiwanja ,mahali- kishiri,tarehe ya mnada 4/2/2021
14) Jina la mdaiwa Anna John,dhamana-nyumba, mahali- katoro, tarehe ya mnada 7/2/2o21
15) Jina la mdaiwa Ramadhani k.Mtenego ,dhamana – kiwanja, mahali- geita ,tarehe ya mnada 7/2/2021
16) Jina la mdaiwa Masumbuko Venas ,dhamana -kiwanja-mahali-kanyama_tarehe ya mnada 25/1/2021
17) Jina la mdaiwa Winfrida Masunga(Amos) ,dhamana-nyumba,mahali-igogo,tarehe ya mnada 4/2/2021
18) Jina la mdaiwa Boniphace Kahana,dhamana-kiwanja,mahali-buhongwa ,tarehe ya mnada 12/2/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888, 40470**
**DODOMA,**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa kati ya tarehe **25/1/2021 na 28/1/2021** Kampuni ya **Bonite Bottlers Limited** itasafirisha mzigo mkubwa (Wide load) kutoka mpaka wa **Holili hadi Bonite Bottlers Limited** kupitia **Shrimatunda.** Namba ya gari: **KBZ903A / ZD4287**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **21.30** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.40** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Mpaka wa Holili hadi Bonite Bottlers Limited kupitia Shrimatunda.** Gari lisafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.44/2017**

**JOSEPHINE KOLINELI MAHENGE::::::::::::::::MDAI**
**Versus**
**ORDAN N.CHAULA:::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**NMB PLC:::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**TROPICAL SEEDS LTD::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**HIGHLANDS AUCTION MART:::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
1. **ORDAN N.CHAULA**
2. **TROPICAL SEEDS LTD**

Fahamu kwamba JOSEPHINE KOLINELI MAHENGE amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 28/01/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 18/12/2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI Wilaya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 270/2020**

**MDAI SAUMU J. MWASHETI**

**MDAIWA RAMADHAN A. MKAHAGWA**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA Tsh. 1,730,000/=.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 25/01 mwaka2021 saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **13/01/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**ISMAIL SHABANI AMRI** anatangaza kupotelewa na kadi tano za gari zenye jina la **QIU CHEN** aina ya **KLUGER** yenye namba za usajili **T 156 DMR,KLUGER T 195 DNH, KLUGER T 632 DNP, KLUGER T 938 DMQ** na **HARRIER T 965 DMT.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/39647/2021.**

# Kinara mtihani kidato cha nne alivyopokewa kifalme Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWANAFUNZI Paul Luziga (17), aliyeongoza kitaifa katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne mwaka jana, amepata mapokezi ya kifalme alipowasili shuleni Panda Hill katika Bonde la Songwe mkoani Mbeya.

Kinara huyo ambaye wakati wa matokeo yakitangazwa na Baraza la Mitihani (NECTA) alikuwa jijini Dar es Salaam, amelazimika kurejea mkoani Mbeya kwa ndege baada ya uongozi wa shule yake kumlipia tiketi ya usafiri huo ya kwenda na kurudi ili wampongeze.

Alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), mwanafunzi huyo alishuhudia maajabu baada ya kukuta magari zaidi ya 20 aina ya Coaster yakiwa yamewabeba wanafunzi wenzake zaidi ya 500 na walimu wao waliofika uwanjani huko kumlaki.

Umati huo wa wanafunzi ambao walibeba mabango yenye ujumbe wa kumpongeza mwamba huyo, ulisababisha baadhi ya wananchi nao kujongea uwanjani huko kushuhudia kinachoendelea.

Shughuli hiyo ilisababisha uwanja huo wa ndege kufurika watu waliohitaji kumwona na hata wasafiri wengine walilazimika kusubiri mpaka umati huo upungue ndipo waondoke.

Kwa mujibu wa taratibu za uwanja huo, ni wanafunzi wachache sana walioruhusiwa kuingia ndani ya jengo la kupokea abiria kumsubiri shujaa huyo, hivyo wengine walilazimika kumsubiria nje.

Luziga aliwasili uwanjani huko kwa ndege ya Shirika la Ndege la Taifa (ATCL) majira ya saa tisa alasiri na kulakiwa na wenyeji wake ambao walikuwa wamejipanga kwa namna ya kipekee kwa ajili ya tukio hilo.




Kinara wa matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne 2020, Paul Luziga, akipunga mkono juu ya gari wakati alipopokelewa na msururu wa magari baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), jijini Mbeya jana, akielekea shuleni Panda Hill kwa ajili ya kupongezwa na walimu pamoja na wanafunzi wa shule hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

### SUTI MAALUM

Wakati kinara huyo anapokewa, baadhi ya wanafunzi waliandaliwa kwa kushonewa suti maalum zenye rangi nyeusi na miwani ya rangi nyeusi zilizowafanya waonekane kama walinzi wa Rais.

Baada ya kushuka kwenye ndege, Luziga alivishwa taji maalum na wanafunzi wenzake lililokuwa na maandishi yaliyosomeka 'Paul Luziga, Tanzania One (T.O) 2020' na kupewa maua maalum kisha akapandishwa kwenye gari maalum lenye paa la wazi tayari kwa safari ya kuelekea shuleni.

Baada ya kupanda kwenye gari huku akipunga mkono na kukunja ngumi kuashiria ushindi, gari lilianza safari, huku likiwa limezungukwa na 'walinzi' hao ambao walikuwa wananing'inia kwenye milango mpaka msafara ulipofika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Msafara huo uliokuwa na magari zaidi ya 20 yakiongozwa na gari la Polisi aina ya Probox, ambalo lilitangulia na kuzuia magari yote katika Barabara Kuu kupisha msafara huo, ulianza safari kuelekea shuleni.

Kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, msafara huo ulielekea katikati ya Mji Mdogo wa Mbalizi ulioko takriban kilometa 10 kutoka uwanjani huko na kuzunguka barabara kadhaa za mji huo kabla ya kurejea shuleni umbali wa zaidi ya kilomita 20.

### KAULI YA MKUU WA SHULE

Akitoa historia ya kitaaluma ya Luziga, Mkuu wa Shule ya Panda Hill, Zephania Lusanika, alisema kijana huyo alikuwa anafanya vizuri tangu kwenye mtihani wa usaili mwaka 2016 ambapo alishika nafasi ya tatu kati ya wanafunzi 800 waliofanya mtihani huo kwa kupata wastani wa 92.

Alisema kijana huyo alidhihirisha zaidi ubora wake kwenye Mtihani wa Kidato cha Pili Mwaka 2018 ambapo alifanya vizuri zaidi kuliko wenzake na kuwa wa kwanza.

Alisema kwenye mtihani wa kujipima wa kidato cha nne, kijana huyo alifaulu kwa kupata daraja la kwanza la alama nane (8), lakini kwenye mtihani wa jimbo, aliongeza juhudi na kupata daraja la kwanza la alama saba (7).

Alisema kuwa kabla ya kufanya mtihani wa taifa, kijana huyo aliwaahidi walimu wake kuwa angefaulu, lakini siyo kwa kiwango ambacho amefikia cha kuwa kinara kitaifa.

"Aliwaahidi walimu wake kuwa atafanya vizuri kwenye mitihani yake na kuwapeleka bungeni jijini Dodoma badala ya Mlimani City jijini Dar es Salaam. Kwa hiyo, tulikuwa tunajua atafanya vizuri ila siyo kwa kiwango hicho," alisema Lusanika.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi wengi na wanafanya vizuri kwa sababu wanalelewa katika mazingira ya kujituma, kuwa na nidhamu na kumtumikia Mungu.

Alisema katika miaka 10 iliyopita shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri na imekuwa miongoni mwa shule 50 bora kitaifa, huku wanafunzi wakijitokeza kwenye orodha ya vinara 10 kwenye matokeo ya kidato cha nne na cha sita.

### MAMA WA SHUJAA

Mama mzazi wa Luziga, Lucy Mogela, alisema alipokea matokeo ya mwanawe huyo kwa mshtuko uliosababisha adondoshe machozi ya furaha kila anapopigiwa simu na watu kumpongeza kuhusu matokeo ya mwanawe.

Alisema Paul ni mtoto wake wa mwisho kuzaliwa kati ya watoto sita na kwamba wote wamesoma, lakini hakuna aliyefaulu kwa kiwango cha juu kama kijana huyo.

Mama huyo ambaye ni mjane, alisema mwanawe huyo alianza kuonyesha kuwa ana akili nyingi wakati akiwa mdogo ambapo alikuwa anahoji maswali mengi ambayo yalikuwa yanaashiria kuwa na upeo mkubwa.

"Kila mzazi anayempeleka mtoto wake shuleni, huwa anatamani mtoto wake afanye vizuri, kwa hiyo mimi nimejawa na furaha kubwa sana na ninaamini ni mpango wa Mungu uliomwezesha mwanangu huyu," alisema Lucy.

Aliwashukuru walimu na walezi wa wanafunzi wa shule hiyo kwa kumlea vyema mwanawe pamoja na wenzake na hivyo kuwafanya kufaulu vizuri kwenye mitihani yao huku akiwataka wanafunzi waliobaki, kumwamini Mungu.

### SIRI YA MAFANIKIO

Akizungumza na wenzake baada ya kulakiwa shuleni huko huku akiwa amezingirwa na walinzi wake, Luziga alisema siri ya kufanya vizuri kwenye mitihani hiyo ni kujituma kwenye masomo na kumtumainia Mungu.

Alisema hata yeye hakutarajia kuwa angefaulu kwa kiwango hicho cha kuwa kinara kitaifa na hivyo matokeo hayo yalimshtua na hakuamini kabisa mwanzoni.

"Ninatamani sana kuwa injinia na ninaamini kuwa nitaweza, ninachoamini ni kwamba siri ya mafanikio yangu ni kujituma pamoja na kumtumainia Mungu, hivyo ninachowashauri wenzangu ni kuongeza bidii na kufuata kile wanachoelekezwa na walimu," alisema Luziga.

Aliwashukuru walimu wake na wanafunzi wenzake kwa mapokezi aliyoyapata kuanzia uwanja wa ndege mpaka shuleni huko, akisisitiza kuwa ni historia kubwa kwenye maisha yake.

### WANAFUNZI WALONGA

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo, walisema matokeo ya Luziga yamekuwa ni changamoto kubwa kwao kwa kuwa yameiletea heshima shule yao ambayo hata wao wanatakiwa kuitetea watakapofanya mitihani.

Mmoja wa wanafunzi hao, Sued Ndanzi, ambaye ni mwanafunzi wa Kidato cha Nne, alisema ufaulu wa kijana huyo unawafanya na wao kuwa na wivu wa kutaka wafanye vizuri na kufanyiwa sherehe kama hiyo.

Alisema wanafunzi wengi huwa wanakuwa na uwezo, lakini wanashindwa kufanya vizuri kutokana na kutojituma kwenye masomo na kutozingatia kile wanachofundishwa.

"Walimu wetu wameamua kumfanyia mwenzetu kitu hiki ili kutuhamasisha sisi tuliobaki, wanatueleza kabisa kwamba kila mtu anaweza kuwa T.O (Tanzania One), hivyo tunaamini hii ni hamasa kwetu," alisema Ndazi.

Elizabeth Mwalukana, mwanafunzi mwingine katika shule hiyo, alisema watahakikisha wanamtumia kijana huyo kama dira yao kwa kujituma zaidi kwenye mitihani ya kidato cha nne na cha sita ili kuiendeleza sifa ya shule hiyo.

Aliuomba uongozi wa shule hiyo kuendelea kuwafanyia sherehe wanafunzi wanaofanya vizuri, ili kuendelea kuweka hamasa kwa wanafunzi wa shule hiyo kuongeza juhudi.

Kuanzia katika Uwanja wa Ndege mpaka kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Panda Hill, wanafunzi walikuwa wanaimba wimbo wa kumpongeza kijana huyo wakisema 'We T.O! we T.O! we T.O!'

Januari 15, mwaka huu, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alitangaza matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, Kidato cha Pili na Darasa la Nne na kubainisha kuwa Tanzania One kwa Kidato cha Nne ametoka katika shule hiyo ya mkoani Mbeya.

HABARI KITAIFA

## Wavamizi waamriwa kuondoka eneo mgodi

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

NAIBU Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, ameamuru watu waliovamia mgodi wa almasi unaomilikiwa na kampuni ya El Hilal Minerals, eneo la Mwangokolo, Mwadui mkoani Shinyanga, kuondoka ndani ya siku mbili.

Prof. Manya alitoa maagizo hayo juzi alipotembelea eneo hilo na kuitaka Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Shinyanga, kuwaondoa ili kulinda eneo hilo la mwekezaji.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka El Hillal Minerals Limited yenye leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya almasi, kuhusu kuvamiwa na wachimbaji wadogo katika eneo lake.

Awali, katika kikao baina ya uongozi wa wizara na wachimbaji wakubwa wa almasi, wachimbaji wadogo pamoja na wafanyabiashara wa madini, Prof. Manya alitoa maelekezo maalumu akiwataka kusitisha utaratibu wa kuendelea kudhamini vikundi mbalimbali vya wachimbaji wadogo kuvamia kwenye eneo lenye leseni na kushauri wazingatie sheria za madini kwa faida ya pande zote.

"Ninaelekeza wachimbaji wote waliovamia eneo hili la mgodi kuondoka ndani ya siku mbili kwa kuwa mnafanya shughuli za madini kinyume cha sheria," amesema Naibu Waziri.

Prof. Manya alisema wawekezaji wajitokeze kwa wingi kwa kuwa ni lazima serikali ilinde haki za wachimbaji wakumbwa, wadogo na wakati.

"Sheria ya Madini inasema mwenye leseni anao wajibu wa kuheshimiwa pamoja na kupatiwa ulinzi na usalama ili afanye shughuli zake ipasavyo.

Aidha, Prof. Manya alimwelekeza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Shinyanga kuhakikisha anaongeza ulinzi na eneo hilo baada ya siku mbili kukamilika kuanzia leo.

"Ninawataka wachimbaji wote mliovamia eneo hili mfuate utaratibu uliopangwa na namwelekeza Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa kuhakikisha anawapatia eneo tofauti ili mwendelee na uchimbaji, lakini mkiwa kwenye taratibu zinazotambulika kisheria," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Teleck, alimpongeza Prof. Manya kwa kutoa maelekezo kwa wachimbaji kuondoka na kuiagiza kamati yake ya ulinzi na usalama ya mkoa kuzingatia maagizo hayo ili kutatua mgogoro huo wa uvamizi.

Naye Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumbulu, alisema kuwa Januari 20, mwaka huu, ofisi ya madini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, iliwatoa zaidi ya wachimbaji wadogo 400 waliovamia eneo lenye leseni ya uchimbaji ya mgodi wa mwekezaji huyo.

# Wataka JPM asipokee ripoti ya ardhi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WANANCHI wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wamemwomba Rais John Magufuli, asikubaliane na mapendekezo ya ripoti ya mchakato wa timu ya ardhi mseto (MLUM) na timu ya mpango wa ujumla wa usimamizi wa eneo hilo, kwa kuwa haina baraka za wenyeji.

Wamesema wapo tayari kutafuta suluhu ila ushirikishwaji uwe wa dhati na usiwe na mashinikizo.

Akisoma tamko la madiwani 11 wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, vijiji 25 na viongozi wa mila wa Tarafa ya Ngorongoro, James Moringe, alisema sehemu kubwa haijashirikishwa na ripoti haikuzingatia maoni ya jamii.

Vile vile, alisema ripoti hiyo imependekeza eneo la wenyeji kutwaliwa, hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya jamii hiyo.

Moringe ambaye ni Diwani wa Kata ya Laitole (CCM), alieleza: "Sisi madiwani na Malaigwanani, kwa niaba ya wenyeji wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, kwa unyenyekevu tunamwomba Mheshimiwa Rais Magufuli atupie jicho eneo hili ili ikiwezekana abadilishe uongozi wa NCAA na kufumua taasisi hiyo kwa sababu imeshindwa kusimamia eneo na ndio chanzo cha mgogoro na kudorora kwa uhusiano kati ya jamii na wahifadhi."

Kabla ya kutolewa tamko hilo, Diwani wa Kakesio (CCM), Johannes Tiamasi, ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Wafugaji nchini, alisisitiza kuwa wenyeji wako tayari kushirikiana na mamlaka katika kutatua matatizo yanayoikumba eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikiwamo uvamizi wa mimea isiyo ya asili, ongezeko la idadi ya watu na maendeleo hafifu ya wenyeji.

"Shughuli za uhifadhi na za utalii zinachangia kwa sehemu kubwa kukuza uchumi wa nchi yetu na hivyo kupunguza umasikini. Wenyeji ni wahifadhi wa asili na wameendelea kuisaidia serikali katika kulinda, kutangaza na kushiriki kutatua matatizo yanayoikumba sekta ya maliasili na utalii," alisema Tiamasi

Aidha, Mwakilishi wa viongozi wa mila wa Tarafa ya Ngorongoro, Lazaro Saitoti, alimuomba Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damasi Ndumbaro asikubali pia kupotoshwa na akubali kukaa upya na wenyeji na kujadili namna ya kutatua matatizo yanayotajwa kuidhoofisha NCCA.

Saitoti alisema wenyeji wa Hifadhi ya Ngorongoro, si wavamizi wa eneo la hifadhi, bali ni wakazi halali wenye haki za msingi na wanaotambulika na sheria iliyoanzisha eneo hilo mwaka 1959.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Iringa, Domina Mukama (kushoto), akikabidhi funguo za nyumba kwa mama mjane Husna Joseph, mjini humo jana, baada ya kujengewa nyumba mpya katika eneo la Kihesa, kutokana na kiwanja walichokuwa wakikimiliki na marehemu mume wake kuuzwa katika mazingira ya kutatanisha. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mjane aliyetapeliwa kiwanja ajengewa nyumba

**Na Francis Godwin,** IRINGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa, imemwezesha mjane Flora Richard, mkazi wa Kihesa, aliyekuwa ametapeliwa kiwanja, kujengewa nyumba ya kisasa na mtuhumiwa anayedaiwa kununua kiwanja hicho pasipo kufuata utaratibu.

Mjane huyo baada ya kuona kiwanja alichokuwa anamiliki, ambacho aliachiwa na marehemu mume wake kimejengwa nyumba na mtu mwingine, alifika ofisi za TAKUKURU kulalamika na taasisi hiyo ilifuatilia na kubaini kuwapo kwa dalili za utapeli.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa, Domina Mukama, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa baada ya TAKUKURU kuingilia kati mgogoro huo, walizikutanisha pande zote mbili zilizokuwa zikivutana na kufikia makubaliano ya kununua kiwanja kingine kwa ajili ya kumjengea mjane huyo.

Mukama alisema nyumba hiyo yenye vyumba vitatu, imekamilika na tayari jana ilikabidhiwa kwa mjane huyo na familia yake tayari kwa kuhamishia makazi yao katika nyumba hiyo.

Bila kumtaja aliyejenga nyumba hiyo, Mukama alisema mtu ambaye amekubali kumjengea nyumba mjane huyo ni mtu wa pili kununua kiwanja hicho, hivyo alilazimika kujitolea kujenga nyumba hiyo ili kuepusha malumbano.

Mjane huyo aliipongeza TAKUKURU kwa kumsaidia kupata haki yake na kuwa sasa ataishi katika nyumba hiyo ya kisasa.

Alisema awali alikuwa akiishi kwa mama yake kutokana na kukosa nyumba ya kuishi ila sasa atalazimika kuishi kwenye nyumba hiyo.

Wakati huo huo, TAKUKURU Mkoa wa Iringa kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, ilipokea malalamiko 57 na baadhi ya mashauri 21 yalifikishwa mahakamani na mengine 18 kuzishauri taasisi husika juu ya nini cha kufanya.

Mukama alisema pamoja na kupokea malalamiko hayo, taasisi hiyo kwa kipindi hicho imeokoa vifaa ghafi vya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambavyo vilitakiwa kurejeshwa na mkandarasi baada ya kukamilisha kazi kama mikataba ilivyomtaka.

Aidha, alisema Sh. 582,619,651.00 zimeokolewa kutokana na ukusanyaji wa madeni kutoka wadaiwa sugu wa SACCOS kwenye vyama vya ushirika, benki na wakopeshaji binafsi katika wilaya zote za mkoa wa Iringa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Timu Ligi Kuu ziache malalamiko, zijipange

**LIGI** Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa imesimama kwa ajili ya kutoa nafasi kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), inayoshiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), inatarajia kuendelea tena ifikapo Februari 19, mwaka huu.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, itaendelea katika mzunguko wa 19.

Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa mzunguko huo, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imetangaza timu za Simba na Namungo FC zitacheza kwanza viporo vyake (mechi tatu kila timu), hii ni kutaka kuona klabu zote zitakuwa zimecheza mechi sawa kabla ya mzunguko wa 19 haujaanza rasmi.

Mabingwa watetezi, Simba ya jijini Dar es Salaam na Namungo ya mkoani Lindi zimekuwa na mechi za viporo kutokana na kubanwa na majukumu na mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Kuelekea mechi hizo za viporo na mzunguko wa pili ambao umeshaanza, Nipashe inazikumbusha timu zote kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kufanya vyema katika mechi zake za hatua ya lala salama.

Timu zitakazojiandaa vizuri, zitajiweka katika nafasi ya kupata matokeo chanya na kujiimarisha kwenye mbio za kuwania ubingwa wa msimu huu, huku zilizokuwa katika hatari ya kushuka nazo zitajinasua na janga hilo.

Tunaamini kila timu kupitia makocha waliowaajiri zijiimarisha kwa kusajili wachezaji wapya kwa lengo la kuongeza nguvu baada ya kubaini upungufu uliyojitokeza wakati wa mzunguko wa kwanza na kuzifanya baadhi ya timu kupoteza idadi kubwa ya michezo.

Baada ya kukamilisha kwa zoezi la usajili wa dirisha dogo, muda ulipo ni timu kuendelea kujiimarisha kwa kufanya mazoezi yatakayowaweka imara kwa ajili ya kupambana kusaka pointi tatu katika kila mechi na hatimaye kutimiza malengo waliyojiwekea.

Tunawashauri timu zote kujipanga kuhakikisha kipenga cha lala salama kitakapoanza, kila upande unafanya majukumu yake na kuepuka kutumia muda mrefu kulalamika au kulaumu na badala yake kutumia nguvu zaidi katika kusaka pointi uwanjani.

Dunia ya sasa pointi hupatikana uwanjani, hakuna mteremko, hakuna miujiza, timu iliyosajili vizuri, iliyojiandaa vyema ndio yenye nafasi ya kutwaa ubingwa ambao bado uko wazi na hata walioko mkiani, pia wana nafasi ya kuondoka huko na kujihakikishia nafasi ya kubakia kwenye ligi hiyo ya juu upande wa Tanzania Bara.

Viongozi, makocha na wachezaji kila mmoja atakapotekeleza vyema majukumu yake, tuna hakika atakuwa ameisaidia klabu yake kwa asilimia kubwa kutimiza malengo yao na kuingilia majukumu ya mwingine, ni kutaka kujiondoa wenyewe kwenye ushindani.

Lakini tunawakumbusha viongozi wa klabu zote zinazoshiriki mashindano yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kutumia njia sahihi za kuwasilisha malalamiko na kuacha tabia ya kuzungumza katika vyombo vya habari 'kiholela' na kujikuta wakijiweka matatani.

Kwa kutumia njia sahihi zilizowekwa, viongozi wa klabu hizo watakuwa wanajiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata haki wanayoilia na kukiuka sheria kwa kujiona wao wako juu ya TFF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Tatizo Stars si kocha, wachezaji ni mfumo

**UMEKUWA** ni kama utamaduni wa baadhi ya mashabiki wa soka hapa nchini kwa sasa kuwa kila Timu ya Taifa (Taifa Stars), inapofanya vibaya, basi 'jumba bovu' linamwangukia kocha mkuu wa timu hiyo.

Tangu timu hiyo ilipokuwa chini ya Marcio Maximo, mambo ni yale yale. Hadi alipokuja Emmanuel Amunike hali iliendelea kuwa hivyo hivyo na hata sasa ambapo inafundishwa na Etienne Ndayiragije hakuna kilichobadilika.

Maximo, ambaye ni Mbrazil aliipeleka Stars kwa mara ya kwanza katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), mwaka 2009 zilizochezwa nchini Ivory Coast, lakini baadaye alionekana hafai, akaondolewa.

Walikuja makocha wengi baadaye ambao nao waliondoka kwa mtindo unaofanana na huo, hadi alipokuja Mnigeria, Amunike.

Huyu naye alifanikiwa kuipeleka Tanzania kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zilizochezwa nchini Misri, mwaka juzi. Baadaye naye hakudumu akatimuliwa.

Sisemi kuwa kocha ambaye ameipatia mafanikio timu asifukuzwe, lakini Watanzania kuwa tabia ya kuwaondoa makocha kwa namna ambayo wanaonekana kama vile hakuna kitu walichofanya.

Sasa hivi ukiangalia kwenye mitandao ya kijamii na mijadala inayoendelea kwenye baadhi ya vipindi vya michezo kuhusu Ndayiragije utashangaa.

Ni kocha huyu huyu ambaye kwa kuteua wachezaji ambao si vipenzi kwa mashabiki wa soka nchini, alifanikiwa kuipeleka Stars kwenye michuano ya CHAN ambayo kwa sasa inaendelea nchini Cameroon.

Hata jinsi Stars ilivyofanikiwa kuingia fainali hizo, utagundua kuwa ni juhudi binafsi za kocha huyo kuchagua wachezaji wenye vipaji ambavyo vinaweza kumsaidia huku akimjumuisha golikipa mkongwe na mzoefu, Juma Kaseja.

Lengo lake la muda mfupi lilikuwa ni Stars ifuzu. Alijua amchukue nani na nani ili atimize lengo. Na kweli alifanikiwa.

Kwa sasa anaonekana kama vile haiwezi Stars, afukuzwe na kutafutwa kocha mwingine. Mimi sikatai Ndayiragije kufukuzwa kwa sababu hatokaa milele. Lakini kumpa lawama kuwa ndiyo sababu ya Stars kutofanya vyema katika mechi ya kwanza kwa kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia, ndiyo napoona hakuna uhalisia.

Kwa baadhi ya Wabongo walivyo, leo kama Stars ikiifunga Namibia, zile kelele zote za Ndayiragije zitapungua na kama itapita kwenye hatua ya makundi, basi kelele na malalamiko yanayoendelea sasa yataisha kabisa.

Zinaweza kuibuka pale timu itakaposhindwa kuchukua Kombe la CHAN. Bado kuna baadhi ya Watanzania wanaamini kuwa Stars ina uwezo mkubwa kisoka kiasi cha kuchukua kombe la michuano hiyo na kama likikosekana tatizo linakuwa ni kocha.

Si kweli. Labda ingekuwa ile Stars ya miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa 1980. Baada ya hapo soka la Tanzania lilishuka sana na sasa ndiyo limeanza kupanda tena taratibu, bado hata Stars ikichukua CHAN siyo kwamba itakuwa soka lake liko juu sana.

Hapo miaka ya katikati kuna sehemu tulikosea. Misingi ya kuzalisha wachezaji wapya ilikiukwa. Hatukupata wachezaji bora tena kama kina Mohamed Rishard Adolf, Peter Tino, Mohamed Salim, Juma Mkambi, Charles Boniface Mkwasa, Thuwein Ally na wengineo.

Mashindano ya soka yalianzia shuleni, vyuoni na hata kwenye mashirika ya umma, kampuni na hata sekta binafsi.

Zamani kila kona ya nchi kulikuwa na viwanja vya kuchezea watoto, lakini baadaye vilipigwa bei na kuwa gereji, kujengwa nyumba, ndiyo maana tunaona wachezaji wengi wa Kibongo hata kwenye CHAN, 'kukontroo' mpira tu inakuwa tatizo. Wachezaji wengi wa Kitanzania wana tatizo la kumiliki mpira na kutulia, huu ndiyo msingi mkubwa wa soka ambao mchezaji anafundishwa utotoni.

Badala yake tunaona wachezaji wetu wakiwa na mpira, utafikiri chini au mpira wenyewe una moto.

Hata wachezaji vipenzi vya mashabiki ambao mashabiki wengi wa soka walitaka kocha awaite, walishawahi kuitwa huko nyuma tatizo ni hilo hilo na hakuna walichofanya.

# RC awaweka mtegoni Ma-DED halmashauri

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amewapa siku tatu wakurugenzi wa halmashauri mkoani hapa kujieleza kwa maandishi ni kwa nini wameshindwa kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Agizo hilo alilitoa Januari 19, mwaka huu, katika Kijiji cha Mollo, wakati akipanda miti ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Upandaji Miti mkoani hapa.

Wangabo alisema mwaka 2015 Makamu wa Rais aliagiza kila halmashauri nchini ipande miti walau milioni 1.5 katika kipindi cha mwaka mzima, lakini agizo hilo limeshindwa kutekelezwa katika halmashauri zote za mkoa wa Rukwa.

Alisema mwaka 2018/2019 halmashauri zote nne za mkoa wa Rukwa zilipanda miti milioni 2.5 sawa na asilimia 43 ya lengo na mwaka uliofuata zilipanda miti milioni 1.5 sawa na asilimia 26, na hali hiyo imekuwa ikishuka kila mwaka.

Wangabo alisema maelezo watakayotoa wakurugenzi hayo yawe ya maandishi pia waambatanishe na mpango kazi wa utekelezaji wa agizo hilo ili mkoa upande miti milioni sita katika kipindi cha mwaka mmoja.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Mazingira mkoani Rukwa, Kapteni (mstaafu) Zeno Nkoswe, alizishauri shule za msingi na sekondari kuanzisha mpango kazi wa upandaji miti ya matunda, hasa miparachichi.

Alisema iwapo kila shule itapanda miche 100 na kuitunza kwa kipindi cha miaka mitatu, inaweza kutoa matunda 500 kila mmoja na kila tunda likiuzwa kwa Sh. 500, watapata Sh. milioni 25 ambazo zitasaidia kuboresha miundombinu ya shule zao.

# DC apiga marufuku uchangishaji lazima madawati

**Na Neema Emmanuel,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Salum Kali, amepiga marufuku walimu wa shule za msingi na sekondari kuwadai watoto michango ya madawati kabla ya kuanza masomo.

Badala yake, amewataka wakuu hao wazungumze na wazazi na walezi kama watakubali kuchangia kwa hiari na si kwa kuwalazimisha.

Kali alitoa agizo hilo jana mjini hapa alipokutana na wakuu wa shule za msingi na wakuu wa shule za sekondari, waratibu wa elimu wa kata na ofisa elimu wa wilaya katika kikao chao cha kazi.

Alisema serikali haimlazimishi mzazi kuchangia madawati badala yake walimu wanapaswa kufanya mazungumza ya hiari na kirafiki kuwashawishi ili wachangie.

"Ofisa elimu na nyie walimu wakuu msizuie wanafunzi kuanza shule na wale waliofaulu kuingia kidato cha kwanza kuzuiwa kuanza masomo kwa kudaiwa madawati," alisema Kali.

Aliwataka walimu kutumia mbinu mbalimbali ikiwamo kushirikisha wazazi na wadau wengine kuwaomba wachangie madawati.

Wilaya ya Magu, alisema imekuwa ya pili kwa ufaulu na kwamba lazima watoto wote waendelee kusoma bila vikwazo vyovyote.

"Ukiitumia lugha nzuri kwa wazazi wanaweza kuchangia sehemu kubwa upatikanaji wa madawati na watoto wakaweza kusoma vizuri," alisema.

Pia mkuu huyo wa wilaya aliwataka walimu kushiriki kwenye ujasiriamali kwa kuuza mifugo kwenye kiwanda cha nyama kilichoko wilayani Magu.

Aliongeza kuwa hakuna kitu kibaya kama mwalimu kuwa ombaomba na kuweka madeni mtaani badala yake wajitahidi kufanya shughuli za kuwaongezea kipato ili waishi vizuri.

Glory Mtui, Ofisa Elimu Wilaya ya Magu, alisema licha ya elimu kutolewa bure, wazazi bado wana jukumu la kuchangia kwa hiari ili kupata madawati katika shule mbalimbali.

Aliongeza kuwa hakuna mwanafunzi yeyote atakayerudishwa nyumbani kwa kushindwa kuchangia madawati.




Mkurugenzi Mkuu wa Precision Air, Patrick Mwanri, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kuanzishwa kwa kituo cha mafunzo ya wahudumu kwenye ndege, baada ya kupata kibali kutoka kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA). Kushoto ni Meneja Ubora wa Kituo hicho, Lucas Mathew. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# PM asema changamoto za mkonge kutatuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itahakikisha changamoto zote zilizokuwa zinawakabili wakulima wa mkonge, ikiwamo kuibiwa mapato hazijirudii.

Aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi baada ya kukagua shamba la mkulima mdogo lililoko Magunga Estate wilayani Korogwe.

Waziri Mkuu alisema miaka ya nyuma Tanzania ilikuwa inashika nafasi ya pili duniani katika kilimo cha mkonge kwa kuzalisha tani 200,000 kwa mwaka ikitanguliwa na Brazil.

Hata hivyo, alisema uzalishaji wa zao hilo ulishuka kutoka tani 200,000 kwa mwaka na hadi tani 39,000 na sasa serikali imedhamiria kuongeza uzalishaji na kufikia tani 150,000 ifikapo 2025.

"Awali wakulima walikuwa wanaibiwa sana jambo ambalo kwa sasa halitojirudia tena kwani serikali imejipanga ipasavyo kuhakikisha mkulima ananufaika, hivyo tulime mkonge unalipa," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alisema awali wakulima wa mkonge walikuwa wakilipwa Sh. 50,000 kwa tani kutokana na kuibiwa na watu wasio waaminifu, lakini baada ya serikali kuingilia kati, bei imeongezeka hadi Sh. milioni nne.

Shigela alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya serikali kuamua kusimamia mwenendo wa biashara ya kilimo cha mkonge na tayari wakulima wameanza kupata tija.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge, Saady Kambona, alisema amepokea zaidi ya maombi 2,000 ya wananchi wanaohitaji mashamba kulima mkonge.

Alisema Bodi imepeleka maombi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kurudishiwa mashamba ambayo yametelekezwa ili wayagawe kwa wananchi.

Kambona alisema kwa sasa hamasa ya kilimo cha mkonge ni kubwa baada ya serikali kuonyesha dhamira ya kulifufua zao hilo na wananchi wengi wamejitokeza wameomba mashamba.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) cha Magunga, Shedrack Lugendo, alisema uzalishaji wa mkonge umekuwa mzuri baada ya chama chao kusimamia na Desemba, mwaka jana, walipata daraja la juu ambalo ni 3L kiasi cha tani mbili baada ya kupita miaka 10.

Kuhusu shamba la mkulima mdogo, Estohim Urio, ambalo Waziri Mkuu alilitembelea, alisema mkulima huyo anamiliki hekta 200 alizopewa na Bodi ya Mkonge.

Mwenyekiti huyo alisema mkulima huyo amepanda hekta 182 ambazo mkonge mkubwa unaovunwa ni hekta 113 na eneo lenye mkonge mdogo ni hekta 69.

# Wasindikaji walilia soko la mchele

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WASINDIKAJI wa mchele wilayani Kahama, wameiomba serikali kuwatafutia soko la mchele la pamoja litakalosaidia kutoa bei elekezi yenye tija kwa wafanyabiashara nchini na wanunuzi wa bidhaa hiyo kutoka nchini za Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC).

Hayo yalibainishwa jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzalisha mchele bora wenye viwango vinavyokidhi ushindani katika soko la ndani na nje ya nchini, yaliyotolewa na Baraza la Mchele Tanzania (RCT), kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti (REPOA) kupitia mradi wa TradeCom II.

Victor Muzo, mfanyabiashara na msindikaji kutoka Shinyanga alisema, kila mmiliki wa mashine ya kusindika mchele ana bei yake ya kuuza hali inayosababisha wateja kutotambua bei sahihi ni ipi na kusababisha bidhaa hiyo kununuliwa kinyemela.

Alisema, ili kuwa na bei ya pamoja ni vyema serikali ikaunda ushirika wa wasindikaji wa mchele kila wilaya zinazolima mpunga ili kuwa na bei moja kama ilivyo kwa wakulima wa zao la pamba na tumbaku pamoja na kusaidia kupata soko la uhakika kutoka nchi za SADC.

"Maisha yetu yameshikiliwa na madalali, wanaotupangia bei hasa tunapopata tenda kubwa, tunashindwa kukataa kwa sababu kila mashine inayosindika mchele ina bei yake, tunaomba serikali kutengeneza ushirika ili tuwe na bei moja na yenye tija," alisema Muzo.

Naye Haroun Msuya alisema, mchele umekuwa ukishuka bei kwa sababu ya ukosefu wa masoko ya uhakikisha ya ndani na nje, awali wateja wao wakubwa walikuwa wafanyabiashara kutoka nchini Rwanda, Kenya, Uganda na Kongo ambayo mipaka imefungwa na walizuiliwa kuja kununua.

Asha Hassani alidai, eneo walipojenga viwanda vya uchakati wa mchele liko mjini kati na halikidhi mahitaji na kuiomba serikali kuwatengea eneo lingine kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa na kuwatafutia mikopo yenye riba nafuu ili kuwekeza zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa RCT, Winnie Bashagi alisema, zao hilo linalochangaia Pato la Taifa kwa asilimia 2.6, hulimwa katika wilaya 64 nchini na zaidi ya kaya asilimia 18 zinanufaika na zao hilo.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Timoth Ndanya, aliwataka wafanyabiashara na wasindikaji wa mchele kutumia kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kusindika mchele katika hali ya ubora, usafi na kutambua soko liko wapi.

Pia, aliwataka kuwa na uhusiano mzuri na wakulima wa zao hilo sehemu zote zinazolima mpunga na kuacha kulima zao hilo kwa kutegemea mvua ambazo hupata mavuno ya wastani wa tani 3.5 kila mwaka huku wakitumia kilimo cha umwagiliaji kupata zaidi ya tani sita za mpunga.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge (kulia), akipokea sehemu ya msaada wa madawati 400 kutoka kwa Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, uliotolewa na benki hiyo jana, kwa ajili ya kusaidia tatizo la uhaba wa madawati jijini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yaridhishwa utendaji NHC

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imeridhishwa na kasi ya utekelezaji miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kulitaka shirika kuboresha ubunifu na mikakati ya makusanyo ya malimbikizo ya madeni ya kodi.

Vilevile, kamati hiyo imeliagiza shirika kufanya ujenzi unaozingatia thamani ya fedha za umma sambamba na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa matengenezo ya majengo ya nyumba za shirika, ili kuinua hadhi ya nyumba.

Kamati hiyo imelitaka shirika kuongeza kasi ya ukusanyaji madeni ya kodi za pango la nyumba sambamba na kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi mbalimbali iliyokabidhiwa kuitekeleza.

Shirika hilo pia limepongeza na kamati hiyo kutokana na kasi kubwa katika utekelezaji miradi ya shirika na ile ya kimkakati, hali iliyolifanya kuaminika na serikali na kuongezewa kazi nyingine zaidi za ujenzi.

Akizungumza juzi katika kikao cha kamati hiyo jijini Dodoma, Mwenyekiti wake, Dk. Pius Chaya, alisema NHC inapaswa kuimarisha kipato chake kwa kuhakikisha inakusanya madeni, ili kuwa na utendaji wenye ufanisi na faida kwa shirika.

"Tumeshuhudia shirika likienda kwa kasi nzuri sana hivi sasa kwa kukamilisha miradi iliyokuwa imekwama na pia kujenga miradi mipya ya kimkakati, lakini sisi maagizo yetu kama kamati, tunawataka muimarishe mikakati ya ukusanyaji kodi ili kufanya shirika letu lisonge mbele," aliagiza.

Alilitaka shirika kuimarisha pia uhusiano na halmashauri mbalimbali ili kupata fursa zaidi kama shirika sambamba na kuzisaidia halmashauri katika masuala yanayohusu ujenzi wa nyumba.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mipango ya shirika kwa kamati katika kikao cha kwanza bungeni.

## Mboga, matunda vyatajwa ni fursa

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

WATANZANIA wameshauriwa kulima kilimo cha mboga na matunda kutokana na kuchukua muda mfupi kupata mavuno na kutoa faida kubwa kifedha.

Baadhi ya wakulima wa mboga mkoani Morogoro walisema hayo walipokuwa wanatoa maoni yao juu ya utafiti uliofanywa na Mtandao wa Wakulima Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF), kama kuna athari zozote kwa wakulima uliporipotiwa ugonjwa wa Covid-19 unaoeneza virusi vya corona.

Wakulima wengi waliohojiwa walidai kutoathiriwa na ugonjwa huo, badala yake wale wanaolima mboga na matunda waliwahimiza wananchi kugeukia kilimo hicho kwani mavuno yake hupatikana muda mfupi baada ya kupanda na kwamba ni lishe muhimu kwa wagonjwa pamoja na kuwa na faida kubwa kifedha.

Landport, mjini Morogoro ambaye kwa takribani miaka mitano amekuwa akilima mchicha na tembele, alisema:

"Kilimo cha mboga kina unafuu mkubwa kiuwekezaji kutokana na gharama zake kuwa chini, mafanikio nayaona maradufu."

Akabainisha zamani alikuwa akijihusisha na ununuzi wa nafaka, lakini hakuwa akipata faida kama alivyotarajia, hivyo kuachana na biashara hiyo na kuamua kulima mboga.

Nao baadhi ya wafanyakazi ndogo katika mashamba ya mboga, Kibua Ali, Haruni Daudi na Ezekiel Kipande walisema shughuli hizo zimekuwa zikiwapatia uhakika wa kipato kila siku na kufanya familia zao kuwa na uhakika wa kuishi na kufanya shughuli zingine za maendeleo zikiwamo elimu, afya na mitaji ya biashara.

## TTCL yatekeleza maagizo ya waziri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL), limeanza kutekeleza baadhi ya maagizo ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, aliyoyatoa hivi karibuni.

Maagizo hayo ni yale yaliyotolewa alipozungumza katika kikao kazi cha shirika hilo kilichojumuisha viongozi wa shirika na mameneja wa mikoa, mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa.

Dk. Ndugulile, moja kati ya maagizo yake, lilikuwa shirika kuendelea kujitangaza, kuboresha bidhaa, kuboresha huduma kwa wateja na kuongeza ubunifu.

Katika utekelezaji huo, baadhi ya watumishi wa shirika hilo wakiongozwa na Meneja Uhusiano, Puyo Nzalayaimisi, wameanza kutangaza bidhaa zao kwa kipindi chote cha Bunge kwenye viwanja vya Bunge jijini hapa.

Huduma zinazotolewa kwa wabunge katika kipindi hicho cha kamati za bunge zinazoendelea ni pamoja na usajili wa laini za simu za TTCL, huduma za T-PESA na uuzaji wa bidhaa zinazotolewa na shirika hilo.

Mmoja wa wabunge waliohudumiwa ni Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima ambaye alilitaka shirika kuendelea kutoa na kuboresha huduma ya mawasiliano katika sekta ya afya nchini.

Nzalayaimisi aliahidi kuendelea kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na waziri ikiwa ni hatua ya shirika kijitangaza na kuleta ushindani katika sekta ya mawasiliano.

"Tutaendelea kutoa huduma zetu zenye viwango bora na kulitangaza shirika letu, ili kufikia malengo pamoja na kutimiza maazimio yaliyotokana na kikao kilichopita," alisema

# Aweso atangaza kuweka kambi DUWASA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema wizara yake itaweka kambi katika ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ili kuhakikisha tatizo la maji linalolikabili jiji linapatiwa ufumbuzi haraka.

Aweso aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake ya kikazi kukagua miradi mbalimbali ya maji inayoendelea kutekelezwa ili kukabiliana na uhaba mkubwa uliopo hivi sasa.

Kwa mujibu wa Aweso, wizara yake kuanzia sasa itapiga kambi katika mamlaka hiyo na kufanya ukaguzi usiku na mchana kukagua miradi ambayo inaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dodoma.

Alisema hivi sasa mkoa wa Dodoma unakabiliwa na uhaba wa maji kutokana na ongezeko la watu katika jiji hilo, pamoja na shughuli za ujenzi zinazoendelea katika maeneo mbalimbali kutokana na ujio wa serikali.

"Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji hivi sasa kwani mpaka sasa tunao uwezo wa kuzalisha lita milioni 66 pekee wakati mahitaji yetu halisi ni lita milioni 103," alisema Waziri Aweso.

Alisema kutokana na hali hiyo, miradi inayotekelezwa hivi sasa ikiwamo ile ya uchimbaji wa visima 15 katika eneo la Mtumba, itasaidia kupunguza uhaba huo itakapokamilika.

Pia alisema hadi hivi sasa visima saba tayari vimeshachimbwa ambavyo vitaongeza lita za maji milioni 21.

Aliwaagiza DUWASA kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha kwa wakati.

"Fanyeni kazi usiku na mchana ili kukamilisha miradi hii. Sisi tutakuwa tunafanya ziara ambazo hazina taarifa iwe usiku au mchana kuona maendeleo na hatutamlea mtu mzembe," alisema.

Akiwa katika mradi wa ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji katika Kata ya Buingili wilayani Chamwino, Aweso alitoa maelezo kuwa mradi huo ukamilike kabla ya Februari 28, mwaka huu.

Akitoa maelezo kuhusu mradi huo wa tangi la maji, Meneja wa Ufundi wa DUWASA, Mhandisi Kashilimu Mayunga, alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Februari mwakani.

Mayunga, alisema tanki hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua lita milioni 2.5 kutoka katika visima mbalimbali vya eneo hilo.

"Mradi huu ukikamilika utakuwa umeondoa kabisa tatizo la maji kwa wakazi wa Wilaya ya Chamwino pamoja na eneo la Ikulu ya Rais," alisema.



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoa wa Dodoma, ACP Anania Amo (kushoto), akipokea zawadi ya jiko la gesi kutoka kwa Mkurugenzi wa kampuni ya Vunjabei, Shija Kamanija, ikiwa ni sehemu ya kurudisha faida kwenye jamii katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vituo vya malezi suluhisho la maadili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

VITUO vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika jamii ndilo suluhisho la kero mbalimbali zinazojitokeza ikiwamo mmomonyoko wa maadili kwa watoto, imeelezwa.

Hali hiyo imeisukuma serikali kuanzisha mradi wa ujenzi wa vituo hivyo unaochangiwa na wananchi wa maeneo husika.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Mtoto kutoka Wizara ya Afya-Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Sebastian Kitiku, aliyasema hayo jana alipokagua ujenzi wa vituo hivyo katika halmashauri za wilaya nne zilizopo mkoani hapa.

Kitiku alisema Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, iliona umuhimu wa vituo hivyo ili kusaidia wazazi na walezi katika maeneo husika kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi huku wakiwa na uhakika wa malezi ya watoto wao.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa vituo hivyo vitamilikiwa na kusimamiwa na jamii husika ambayo pia itakuwa na jukumu la kuanzisha vikundi vya malezi kwa lengo la kuiwezesha jamii kuwa na malezi chanya kwa watoto.

"Hivi vituo vitatusaidia katika kutoa elimu ya malezi kwa wazazi na watoto pia kwani vikundi vya malezi vya wazazi vitaanzishwa ili kuendana na uendeshaji wa vituo hivi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Nkulo, alisema vituo hivyo vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ni muhimu sana katika jamii na vitasaidia jamii kuwa na mahali salama kwa malezi ya watoto.

Alisema hatua hiyo ikiungwa mkono na jamii, itasaidia kuunga mkono juhudi jitihada za serikali kuchochea uchumi wa viwanda ulioiwezesha kufikia uchumi wa kati.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Chamwino, Peter Simba, alisema kituo cha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kijijini hapo ni neema ya pekee kwao, hivyo watahakikisha wanashirikiana na wadau kuharakisha ujenzi wa kituo hicho ili kitoe huduma inayokusudiwa.

Ofisa Mradi kutoka Shirika la Brac, Pius Ulaya, alisema shirika linaunga mkono juhudi za serikali za kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi wake kupitia ujenzi wa vituo hivyo katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, ili kusaidia jamii kuondokana na kero ya watoto kukosa sehemu sahihi za kujifunza na kupata malezi pale wazazi wanapokuwa katika shughuli za maendeleo.





## Alonga na idara wenye ulemavu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ametembelea Idara ya Watu Wenye Ulemavu, iliyo chini ya ofisi yake na kuzungumza na watendaji wake, kubadilishana mawazo na kujua changamoto zinazowakabili.

Katika ziara yake hiyo juzi, Maalim Seif alisema jamii haipaswi kuwadharau wala kuwatenga watu wenye ulemavu kwa kuwa yeyote ni mwenye ulemavu mtarajiwa.

''Katiba yetu ya Zanzibar inakataa ubaguzi wa aina yoyote ile, hivyo ni kosa kuwabagua watu wenye ulemavu kwani wanastahili kuheshimiwa na kupewa haki zao zote,'' alisema.

Pia alisema inahitajika elimu kwa jamii juu ya ulemavu kwa kuwa wako baadhi ya watu wanaodhani kuzaa mtoto mwenye ulemavu ni mkosi au laana, hivyo kusababisha kuwaficha na kuwakosesha haki zao za msingi.

Alisema kuna haja ya majengo yote ya biashara au ya kutoa huduma yoyote, yawape vipaumbele watu wenye ulemavu katika kujenga miundombinu ya kuwasaidia kufikia huduma hizo.

Maalim Seif alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mjini, kuwadhibiti wale wote wanaowatumia wenye ulemavu kuomba pesa barabarani kwa ajili ya kuwanufaisha na kuwafanya kama kitega uchumi.

Alisema ziko taarifa kwamba watu wanawachukua wenye ulemavu na kuwaleta Zanzibar kwa ajili ya kuwatumikisha. Hata hivyo, alisema hakatazwi mgeni kuja Zanzibar, lakini si kuombaomba, hivyo ni kuwadhalilisha walemavu na jambo hilo halipaswi kuvumiliwa.

Mkurugenzi wa Idara hiyo, Abeda Rashid Abdallah, alisema miongoni mwa majukumu ya idara ni kusimamia upatikanaji wa haki na usawa kwa watu wenye ulemavu na kusaidia na kusimamia mikataba ya watu wenye ulemavu.

# Maalim Seif atoboa siri viongozi CCM kutokuwa na dhamira SUK



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, akisalimiana na Mkurugenzi wa Idara ya Watu wenye Ulemavu, Abeda Rashid Abdallah, alipofanya ziara katika ofisi za idara hiyo, eneo la Mazizini, Unguja juzi. **PICHA: OMKR-ZNZ**

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT -Wazalendo, na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ametoa siri kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ya 2010- 2015 haikuwa mioyoni mwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Maalim Seif aliyasema hayo huko Kizimkazi Mkunguni Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja alipokutana na viongozi na wanachama wa ACT- Wazalendo kutoka mkoa wa Kati Unguja na mkoa wa Kusini Unguja kichama.

Alisema hayo alipokuwa akijibu maswali baada ya kutoa fursa kwa wanachama kuuliza na kutoa maoni yao. Baadhi ya wanachama walionyesha hofu ya uwapo wa SUK wakisema kabla ilishakuwapo lakini faida yake haikuonekana.

"Kwa hakika viongozi wa CCM ambao tuliunda nao Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyoanza 2010 mpaka 2015, walifanya hivyo ili tu kutimiza matakwa ya kikatiba ila mioyoni mwao hawakulitaka," alisema.

Maalim amewatoa hofu wanachama hao kwamba: "Kwa siku hizi 43 ambazo mimi nimeanza rasmi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, nimeona wazi dhamira ya kweli ya Rais (Dk. (Hussein) Mwinyi juu ya uwapo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tunakaa pamoja, tunaongea, tunashauriana na tunaona yanatekelezwa na hii ni ishara njema juu ya umoja na mashirikiano (ushirikiano) tunayoyataka (tunaoutaka) Wazanzibari."

Maalim Seif alisema serikali kwa sasa inatakiwa kufanya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ili ipate mpya ambayo itarekebisha kasoro zilizopo.

"Tukipata Katiba mpya ya Zanzibar basi ndani yake tutapata Tume Huru ya Uchaguzi, tutapata majaji wa mahakama walio huru na watakaotenda haki," alisema.

Alisisitiza kuwa: "Mimi ni Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo nikiwa katika shughuli za chama, lakini mimi ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, hivyo nitahakikisha kila Mzanzibari anapata haki yake bila kuangalia itikadi ya chama chake ikiwa tu ni Mzanzibari."

Alisema huu ni muda wa kufanya siasa na kuboresha chama, hivyo ni lazima wote kwa pamoja washirikiane kuanzia ngazi ya tawi mpaka taifa, kufanya majukumu ya kitaasisi sambamba na kuelekea uchaguzi mkuu 2025. Pia aliahidi kushuka katika matawi kuangalia utendaji.

# Dk. Mwinyi aweka wazi umuhimu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema Serikali ya Umoja wa Kitaifa imedhamiria kuendeleza amani, umoja na mshikamano kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambayo inakwenda sambamba na misingi ya Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF).

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa MNF, ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Joseph Butiku, Ikulu Zanzibar.

Uongozi wa taasisi hiyo ulifika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kumpongeza Dk. Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar pamoja na kuendeleza Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa SUK kumeimarisha amani, umoja na mshikamano Zanzibar hatua ambayo ni chachu ya maendeleo na imekuwa ikisisitizwa siku zote na MNF.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na maelewano na ushirikiano mkubwa kati ya viongozi na wananchi wengi wa Zanzibar hali ambayo imesababisha kuimarika kwa umoja, amani na mshikamano tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Rais Mwinyi aliongeza kuwa hatua hiyo imefikiwa kutokana na maridhiano yaliyofanyika ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa SUK ambayo lengo na madhumuni yake ni kuendeleza umoja, amani na mshikamano ili Zanzibar izidi kupata maendeleo na wananchi wake wazidi kuelewana.

Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuipongeza MNF kwa kufanya kazi kubwa na nzuri ndani na nje ya nchi pamoja na jumuiya ya kimataifa.

Taasisi hiyo, alisema imekuwa na uhusiano mzuri na serikali zote mbili, ushirikiano na taasisi za kidini na vyama vya siasa. Pia alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano wa pamoja na wenye kuleta tija.

Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kueleza kwamba taasisi zisizo za kiserikali (NGO) zina dhima kubwa ya kuwaletea wananchi maendeleo badala ya kujikita zaidi katika masuala ya kisiasa.

Alisisitiza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane itaendelea kutoa ushirikiano wake kwa taasisi hiyo pamoja na zingine nchini katika kuhakikisha malengo yaliokusudiwa yanafikiwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha umoja, amani na mshikamano kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Awali, Butiku alimweleza Dk. Mwinyi azma ya ujio wao ikiwa ni pamoja na kumpongeza kwa kuchaguliwa kwa kishindo na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar katika uchaguzi uliofanyika mwaka jana.

Pia taasisi hiyo ilimpongeza Dk. Mwinyi kwa kuwezesha kuendeleza tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa SUK kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa lengo la kufikia demokrasia ya hali juu na maendeleo.

Butiku alisema kwamba hivi sasa Zanzibar imeonekana ikiwa na amani, umoja, utulivu na mshikamano mkubwa kutokana na maridhiano yaliyofanyika.



**ALI KIBA AONA USHAMBA KUVAA HERENI** Ukurasa 12

JUMAMOSI JANUARI 23, 2021

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



### UPWEKE WAMZONGA

# Queen Darleen kusuka au...

SAKATA la uhalali wa baba mzazi wa mwanamuziki maarufu nchini, Diamond, linazidi kuwaumiza vichwa mashabiki wa Bongofleva na kusababisha kuwapo na maswali mengi kuliko majibu.

Wiki iliyopita, mama mzazi wa msanii huyo, Sandra Kassim, maarufu mama Dangote, alimtaja baba mzazi wa Diamond Platnumz kuwa ni Salum Idd Nyange na sio mzee Abdul ambaye anajulikana na wengi.

Licha ya tukio hilo kuitikisa nchi kutokana na uzito wake, lakini imeitetereshа familia hiyo hasa baada ya kutajwa msanii Queen Darleen, kuwa hana undugu na Diamond licha ya kulelewa na mama huyo.

Hata hivyo, hakuna aliyejitokeza kuzungumzia suala hilo kati ya Diamond na Queen Daleen, hivyo kuibua wasiwasi kwamba ndani ya familia hiyo maarufu kuna mpasuko mkubwa.

Mwimbaji huyo wa kike amekuwa miongoni ma wasanii wa lebo ya WCB kwa muda mrefu, na uwepo wake umeonekana kuwa wa kindugu zaidi kuliko kazi.

Baadhi ya watu wanadai, kutajwa kwamba hana uhusiano wa kinasaba na Diamond ambao awali ilijulikana kama wamechangia baba mmoja, kunaweza kuibua tukio lingine ambalo linaweza kuleta mtafaruku.

Ni wazi watu wanatarajia kuona tamasha la muziki la wasafi linalofanyika jijini Dar Salaam kama Queen Daleen, atatokea jukwaani kutoa burudani, na kama hakutokea basi dalili ya kwanza kwamba mwimbaji huyo yupo mbioni kujitoa inaweza kuaminika.

Watu walio karibu na msanii huyo, wamedai tangu kutokea kwa sakata hilo, yupo kimya lakini amekuwa na mawazo mengi.

"Queen Daleen amevunjika moyo, alikuwa anajivunia watu kuamini Diamond ni kaka yake, lakini kutokana na mama Dangote kuweka wazi, amejikuta mpweke zaidi," amesema chanzo hicho.

BASI SAWA



## Giny hakutarajia mapokezi ya nguvu

MSANII wa muziki wa kizazi kipya anayekuja kasi, Joshen Adam, maarufu kama 'Giny' amesema hakutarajia kama wimbo wake 'Giny Baba' kama utakuwa mkubwa kama ulivyo sasa.

Amesema wimbo huo ambao ameutambulisha mwezi uliopita umepata mapokezi mazuri kwa mashabiki na unampa moyo wa kuandaa ngoma nyingine kali ili kuongeza furaha yao.

"Nashukuru Mungu wimbo wangu umepokelewa kwa nguvu kinyume na nilivyotarajia, nashukuru sana kwa upendo wanaonyesha mashabiki wangu na inanipa nguvu ya kuandaa ngoma nyingine ili nizidi kuwafurahisha," amesema.

## Profesa Jay akerwa kuyaanika ya kitandani

ALIYEKUWA Mbunge wa Mikumi na mwanamuziki, Profesa Jay, amewashauri wasanii wa muziki wa Bongo Fleva kuacha kuimba matusi na mambo ya kitandani.

Profesa Jay amefanya kolabo na rapa Stamina katika wimbo wa 'One Six', kuna umuhimu wa kuokoa kizazi kwa kuepuka kuimba nyimbo zenye maneno ya aina hiyo kwani inawashusha.

"Sio lazima kila siku uimbe matusi na mambo ya kitandani ili wimbo wako uwe mkubwa na upendwe, bali unaweza kuimba wimbo wenye mafunzo mema kwa jamii na wadau wakakushika mkono kwa kiwango cha juu kabisa," amesema.





# Ali Kiba aona ushamba kuvaa hereni

HATIMAYE mwanamuziki nyota wa Bongofleva Alikiba, amesema kamwe hasumbuki na suala la uvaaji wa hereni masikioni kwa sababu muda huo umepita kwake.

''Mambo ya kuvaa sijui hereni masikioni na vitu vingine vya aina hiyo, nadhani kwangu muda wake ulishapita. Hata mitindo yangu ya sasa kuanzia uvaaji wangu kwenye video nadhani unafaa kwa sababu watu wanaohusika na ubunifu wanafanya kazi yao," Alikiba.

Aidha, amesema hakuna kitu ambacho kinaweza kumsumbua akili yake kutokana na mambo mengi amefanya na sasa ameyaacha.



# Monalisa umeyataka lakini...

MWIGIZAJI wa filamu nchini, Yvonne Cherrie, maarufu kwa jina la Monalisa, ameibua gumzo wiki hii baada ya kuwajia juu watu wanaomsakama kuwa watoto wake kazaa na wanaume tofauti.

Mara alipoposti ujumbe huo, baadhi ya mashabiki wamemlaumu kwa maneno yake hayo na kueleza anatoa funzo baya kwa jamii.

Wamemshauri kwamba kutokana na umaarufu wake, watu wengi wanajifunza kutoka kwake, hivyo kauli yake kuwa anaona ufahari kuwa na watoto baba tofauti inaweza kuleta ukakasi wa kimaadili katika jamii.

Katika ujumbe wake huo kupitia akaunti yake ya Instagram, Monalisa alisema ""Sioni haya hata kidogo tena najivunia kuwa mama wa watoto hawa na kutangaza hadharani kwamba kila mtoto ana baba yake, na baba zao wanajijua na ni baba zao hasa," ameandika Monalisa.

# Vita ya familia, chanzo cha moto ni cheche

**Na Adam Fungamwango**

VITA ya familia ni filamu ya aina yake inayoonyesha kuwa wakati mwingine ugomvi wa familia huanzia mbali. Unaweza kuona ukoo mmoja na mwingine unagombana, lakini tatizo lilianzia mbali na si kwa hao wanaogombana. Wakati mwingine inakuwa ni kulipiziana kiasi kwa ugomvi uliotokea kizazi kilichopita, au hata vizazi viwili au vitatu kutoka hapo.

Mtunzi wa filamu hii, alitaka kuikumbusha jamii kuwa wanapoona familia au ukoo unagombana na wanapotaka kusuluhisha, basi waanzie nyuma ili kugundua chanzo ni nini.

Imechezwa na wasanii Salum hamisi, Jackson Mayunga, Aisha Rajab, Angel Nicolaus, Karim Kitwana, Mariam Idd, Mary Damas na wengineo.

Inaanza kumwonyesha Mayunga akiwa nje ya nyumba yao. Lakini anapita mtu mmoja anayeonekana kama kichaa na kumuomba chakula.

Mayunga anampa chakula. Anavyomuona kuwa mtu yule si kichaa, ila maisha magumu ndiyo yamesababisha vile. Hata anavyoongea ilionekana ni kijana mwenye akili zake. Mayunga anaanza kumwamini kijana yule aliyeitwa Karim na kumshirikisha kwenye ushauri wa mambo ya kifamilia.

Mayunga ni mtoto wa mke mdogo kwenye familia hiyo. Hata hivyo baba na mama yake walishafariki, hivyo analelewa na mke mkubwa.

Mke mkubwa yeye alikuwa na watoto Salum Aisha na Mamu. Mke mkubwa alijitahidi kuwalea kwa uzazi sawa, lakini kwa Mayunga aliona kama anaonewa.

Akaenda kwa mganga ili amuue mama yake mkubwa, halafu baadaye amuua Salum ili yeye awe mtawala wa nyumba ile.

Anafanikiwa kumuua mama yake mkubwa. Hata hivyo, tuhuma zinamwangukia Salum ambaye yeye alikutwa chooni alikokwenda kwa jitihada za kutaka kumuokoa mama yake mzazi, ikashindikana. Kila mmoja akadhani yeye ni muuaji. Akatoroka. Aliporeja akawa taahira. Polisi wakakataa kumkamata.

Mayunga tayari nyumba alikuwa ameishika. Ameitawala. Wote wameshawaweza. Amebaki na kinadada tu.

Siku moja analetewa barua. Anaisoma machozi yanaanza kumtoka. Kumbe alidanganywa na yule kijana Karim ambaye alimtumia tu ili amuue yule mama kwa sababu ana kisasi naye.

Kisa ni kwamba, mama yule aitwaye Zubeda ndiye aliyesababisha mama yake Karim aachwe na kuolewa yeye, baada ya wote kupewa mimba na mwalimu mmoja.

Mama yule alipomzaa Karim alifariki, lakini aliacha ujumbe ambapo ulitumiwa na Karim kulipiza kisasi kwa kumtumia Mayunga.






# Filamu ya wazazi wa Diamond inaanzia hapa

**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya mjini kwa sasa ni juu ya mama Diamond na mzee Abdul Juma, kuhusu uhalali wa mtoto Naseeb Abdul maarufu kama Diamond Platinumz.

Sakata hili ndilo limeibua jina la mzee Nyange. Hivi sasa kila mmoja mtaani akiona vipi anajiita mzee Nyange.

Siko hapa kulizungumzia sakata zima jinsi lilivyo kwani limeshazungumzwa na kuandikwa sana kwenye vyombo mbalimbali vya habari pamoja na mitandao ya kijamiii.

Ninachokizungumza hapa ni kwamba mambo haya yapo sana kwenye jamii yetu hasa hizi za Kiafrika. Ndiyo maana wakati wa sakata hili, wapo watu waliokuwa wakieleza ushuhuda wao ambayo yaliwakuta kama hayo kwenye safari zao za maisha.

Wanawake walielezea jinsi walivyoachwa na waume zao wa watoto. Wakawa na kazi ya kulea watoto hadi walipokuwa wakubwa na ndiyo baba zao wakarejea.

Wengine waliwakataa kabisa watoto, lakini walipokuwa wakubwa na kazi zao na uwezo, wakaanza kujisogeza.

Hata wanaume nao walielezea jinsi walivyolea watoto tangu wadogo, lakini baada ya kuwa wakubwa wakiwa wameshastaafu hadi kazi, ndiyo wanakuja kuambiwa kuwa wale hawakuwa watoto zao halisi,

Hapa tunawaletea nyimbo ambazo wanamuziki waliangalia viashiria kwa matatizo ambayo yanaweza kusababisha yanayojitokeza sasa kama hatua za mwanzo hazijachukuliwa.

**Ule Baba Watoto - Lovy Longomba**

Mwanamuziki Lovy Longomba, katikati ya miaka ya 1980, aliimba wimbo uitwao 'Ule Baba Watoto.'

Ni kwamba Ule alimuacha mkewe na watoto wanateseka, akahama nyumbani akawa anaishi kwenye nyumba za starehe, akiiacha familia yake inateseka. Hapo sasa mkewe analalamika juu ya kuachwa na mumewe, akimuachia jukumu la kuilea familia. Huyu baba yanaweza kumkuta mbele ya safari akalalamika.

**Mama Watoto-Les Wanyika**

Kwenye wimbo huu ni kwamba mwanamke ameondoka nyumbani na kumwachia mwanaume watoto.

Sasa mume anapelekewa ujumbe, kama wa barua au wa simu sijui. Lakini anamwambia kuwa arejee nyumbani ili alee watoto. Kwenda kazini, halafu akiwa na jukumu la kulea watoto yeye kwake limekuwa gumu. Mama huyu naye anaweza baadaye kudhani watoto wake hawampendi.

**Mama Feli - Cosmas Chidumule**

Ni mwanaume anayemtoa wasiwasi mkewe kuwa tetesi anazozisikia kama anataka kuoa mke mwingine si kwa ukweli. Anamwambia mkewe kuwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu familia itasambaratika na malezi ya watoto yatakuwa si mazuri.

Mara zote furaha ya watoto ni kuona baba na mama wapo pamoja, lakini hali inapokuwa tofauti, watoto nao wasambaratika na kulelewa upande mmoja.

Hii inasababisha hata watoto wenyewe kuegemea upande mmoja ule ambao amelelewa na kusahau upande mwingine wa mzazi.

**Mundinde - Hemed Maneti**

Kwenye wimbo huu, Maneti akiwa na Vijana Jazz anakwenda kumpasha jirani yake mmoja juu ya vitendo vya kwenda kumwambia maneno maneno mkewe.



# Omotola awaka kuzushiwa kuchepuka

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu kutoka Nigeria, Omotola Jalade Ekeinde, amekuja juu baada ya mwandishi mmoja kufichua siri kuwa anatoka kimapenzi na mwanasiasa wa chama tawala cha APC, Adams Oshiomhole.

Mwandishi huyo wa blog, Gistlover, aliandika kwamba msanii huyo anayefahamika nchini huyo ana uhusiano wa siri na mwanasiasa huyo.

"Huwezi kufanya hivi kabla ya kufikiria kwanza na kupata maoni kila upande, hii blogu imetoa taarifa hizi za uongo na watu wanakuja katika ukurasa wangu. Taarifa si za kweli," amesema.



## Wayne amkubali Trump akiondoka

WAKATI dunia inamwangalia Rais mstaafu wa Marekani, Donald Trump, kama kiongozi mbaya na asiyefaa, lakini wasanii wa muziki wa kufokafoka, Lil Wayne na Kodak Black wanamuona katika jicho lingine.

Wanamuziki hao wamemiuta Trump kama kiongozi mashuhuri na kumuona kama mzazi mlezi kutokana na kitendo chake cha kuwafutia hukumu ya kifungo siku za mwisho wa utawala wake.

Katika ujumbe waliotupia katika kurasa zao za Instagram, wasanii hao wameonekana kuwa na hisia za upendo kwa kiongozi huyo na kumuona kama mtu shujaa na anayetakiwa kuheshimiwa miaka yote.

## Huyu ndiye Amanda

AMANDA Gorman (22) ameingia katika kitabu cha kumbukumbu baada ya kuwa mshairi wa kwanza mdogo kuimba katika sherehe ya kumwapisha Rais wa Marekani.

Kupitia shauri lake The Hill We Climb', Amanda amepata umaarufu duniani baada ya kukonga nyoyo za watu waliohudhuria katika sherehe ya kumwapisha Joe Biden katika jengo la Capital Hill jijini Washington DC.

Kabla ya kuhudhuria, Amanda alipiga kelele na kucheza kama mtu aliyechanganyikiwa pale alipofahamishwa kuwa amechaguliwa kusoma mojawapo ya mashairi yake katika sherehe ya kuapishwa kwa Rais Biden.





## Rotimi, Vanessa wafunga ndoa?

SASA inaonekana kama msanii wa filamu wa Marekani mwenye asili ya Nigeria, Rotimi na mchumba wake Vanessa Mdee, wamefunga ndoa.

Wapenzi hao ambao walivishana pete ya uchumba mwezi Desemba mwaka jana, wamezidi kuleta utata baada ya Vanessa kubadili jina lake na kujiita Mrs 'A' akiashiria tayari amekuwa mke.

Katika kinachoonekana wasanii hao wamefunga ndoa ya siri baada ya Vanessa kuonekana amevaa pete ya ndoa badala ya ile ya awali ya uchumba.

## Teebillz atapika nyongo

MENEJA wa wanamuziki maarufu Nigeria, Tunji Balogun, ambaye anajulikana kama Teebillz, amemtuhumu waziri mstaafu Femi Fani-Kayode, kwa kumuunga mkono aliyekuwa Rais wa Marekani Donald Trump.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter kiongozi huyo alichapisha picha ambayo ilimuonyesha Trump akiaga.

"Umesimama kwa shetani, pigana kwa pigano zuri na simamia katika mwanga wa Dunia, hakuna mtu atakayekuwa nyuma yako," Teebillz ameandika.



MAKALA

# SANDUKU LA NYUKLIA

## •Trump akataa kumkabidhi Joe Biden
## •Changamoto iliyoibua hofu Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya tukio la kuvutia, lakini halifanyiki hadharani ni lile la makabidhiano ya masanduku ya nyuklia kati ya Rais wa Marekani anayeondoka na Rais anayeingia madarakani.

Katika miongo sita wakati wa kuapishwa kwa rais mpya kila Januari 20 baada ya uchaguzi, hafla inayofichwa na shamrashamra zinazoendelea, wanajeshi wawili waliovalia sare zao za kijeshi wamekuwa wamesimama pembeni wakati wa uapishwaji.

Askari mmoja ambaye ni mpambe wa rais anayeondoka madarakani, hubeba sanduku zito ambalo humkabidhi askari mwingine ambaye atakuwa akiandamana na rais mpya.

Sanduku hilo ndilo inaloitwa 'Black Box' au 'Sanduku la nyuklia', ambalo limetengenezwa kwa chuma na kila mahali anapokwenda Rais wa Marekani, uandamana nalo ili kumpatia nafasi kuamuru kurusha bomu la kinyuklia akiwa nje ya ikulu ya White House.

Tangu sanduku hilo lilipoanza kutumika wakati wa utawala wa John F Kennedy, ubebaji wa sanduku hilo umekuwa kitu muhimu, licha ya kutokuwa miongoni mwa vitu vya kipekee katika sherehe hiyo ya kuapishwa Rais.

Hata hivyo, mwaka huu kwa mara ya kwanza njia ya kukabidhi sanduku hilo kutoka mkono mmoja hadi mwingine, haikufanyika tangu kubuniwa kwake zaidi ya karne moja.

Makabidhiano hayo hayakufanyika kutokana na kiongozi anayeondoka Donald Trump, kukataa kuhudhuria hafla ya kumwapisha Rais mpya Joe Biden.

Kulingana na itifaki, Trump alipaswa kuwa na sanduku hilo la nyuklia hadi saa sita.

Lakini ilipofikia muda huo, Trump tayari alikuwa umbali wa kilomita 1,500, kusini mwa Florida na kumuacha Rais Biden peke yake.

Hata hivyo, kuna masunduku mengine kama hayo ambayo yamewekwa tayari kutumika katika makabidhiano endapo kiongozi anayepaswa kukabidhi hayupo.

Swali muhimu ni kwamba makabidhiana ya sanduku hilo la kinyuklia ilifanyika vipi iwapo marais hao walikuwa maeneo tofauti?



Mwanajeshi anayeambatana na Rais wa Marekani akishuka na sanduku la nyuklia kutoka ndani ya ndege.




Mwonekano halisi wa masanduku ya nyuklia. **PICHA: MTANDAO**

### SULUHU ISIYO YA KAWAIDA

Wasiwasi wa jinsi gani sanduku hilo la nyuklia lingekabidhiwa kwa utawala wa Biden, ulijibiwa na Idara ya Ulinzi nchini Marekani, iliyopo Pentagon kuwa ilikuwa na mpango huo siku ya kuapishwa kwa rais mpya, lakini ikakataa kutoa maelezo.

Hata hivyo, wataalamu kadhaa na wasomi wameeleza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika iwapo hali hiyo isiyo ya kawaida itaikumba Marekani.

Stephen Schwartz, amesema tofauti na fikra za wengi, kuna masunduku matatu ya aina hiyo.

Moja ni lile linaloandamana na rais, lakini kuna masanduku mengine mawili ambayo ya dharura yanakuwa kwa makamu wa rais au mtu aliyepewa mamlaka ili kuzuia tukio lolote kama viongozi hao wa juu wamefariki.

Schwartz amesema Pentagon inaweza kutumia mojawapo ya masunduku yake, au kuandaa jipya ili kumkabidhi Biden baada ya kuapishwa. GES

Wakati huo sanduku hilo jipya linakabidhiwa kwa Biden, lile ambalo alikabidhiwa Trump ambalo hakukabidhi linakuwa limeisha kazi yake.

Kutokana na hatua hiyo, kadi zake zinazotoa nambari za siri za sanduku hilo la nyuklia huzimwa.

"Iwapo ofisa anayebeba sanduku hilo aliaandamana na Trump, katika ndege ya Airforce One kuelekea Florida, msaidizi huyo aliondoka mahali alipo Trump, ilipofikia muda wa sita kamili na kurudi Washington na sanduku hilo, ameeleza Schwartz wakati akiiambia CNN.

### SANDUKU LA SIRI

Suala la sanduku hilo limezua maswali mengi na jinsi matumizi yake yamewavutia mamilioni ya watu kwa miaka mingi.

Kile ambacho watu hawakijui ni kwamba namba za siri na funguo zake ambazo zinamruhusu kiongozi wa Taifa hilo kuwa na uwezo wa kutoa maagizo ya kutekeleza shambulio hazipo ndani ya sanduku hilo.

Funguo hizo ambazo zina uwezo wa kutekeleza shambulio la kinyuklia, huwa ni kadi ndogo ya plastiki ambayo rais aliye madarakani hubeba mfukoni.

Kadi hiyo hujulikana kama "Code of Gold au Cookie".

Rais hutakiwa kuikata mara mbili ili kuthibitisha utambulisho wake pale anapowasiliana na kitengo cha vita katika Pentagon, ili kuruhusu shambulio.

Mapema siku ya kuapishwa kwa rais mpya na makamu wake, hupokea maagizo ya jinsi ya kutumia sanduku hilo na rais anayechukua mamlaka hupatiwa kadi hiyo.

Kulingana na jarida la sayansi ya atomiki, Pentagon huzima kadi ya rais anayeondoka madarakani saa sita mchana baada ya kuapishwa kwa rais mpya, huku kadi ya kiongozi ikiwashwa.

Hivyo basi, saa 6:01 ya Januari 20, iwapo Trump angetaka kutekeleza shambulio la kinyuklia, asingeweza kufanya hivyo, licha ya kumiliki sanduku hilo na Biden naye asingeweza kufanya hivyo saa 5: 59 asubuhi.

Hofu iliibuka kuwa Trump angetekeleza shambulio la nyuklia kabla ya kuondoka kufuatia ghasia za uvamizi wa jengo la bunge la Capitol Hill mapema mwezi huu.

Wakati huo, kiongozi wa bunge hilo, Nancy Pelosi, aliwasiliana na idara ya ulinzi na kuwataka kutofuata maagizo ya Trump iwapo angetaka kutekeleza shambulio hilo kabla ya kuondoka katika Ikulu ya White House.

### SANDUKU LILIVYO

Bruce Blair, ambaye alikuwa askari mstaafu wa kutekeleza shambulio la nyuklia nchini Marekani, alielezea BBC, kwamba tofauti na jinsi watu wanavyoamini, sanduku hilo la nyuklia halina kitufe au namba za siri zinazomwezesha rais kutekeleza shambulio la nyuklia moja kwa moja.

Amesema badala yake itifaki za shambulio hilo ni sharti awasiliane na washauri wa ngazi za juu.

"Katika sanduku hilo pia kuna mchoro wa mpango wa vita, malengo yake pamoja na idadi ya watakaofariki bila kusahau silaha zilizopo. "Hivyo ni rahisi kuelewa hali ilivyo katika sekunde chache," amesema Blair.

Ndani ya sanduku hilo sio namba za siri pekee zinahifadhiwa, pia kuna vitabu viwili ambavyo ni muhimu.

Kimoja kina maelezo ya kina kuhusu aina ya shambulio hilo la nyuklia ambalo linaweza kutekelezwa, orodha nyingine ya maeneo salama kwa rais.

Muda wote sanduku hilo huonekana na antena iliojitokeza ambayo hutumika kuimarisha mawasiliano ya moja kwa moja na idara ya ulinzi ya Pentagon.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**

MAKALA

# KWANINI WENGI WANAITAFSIRI JANUARI MWEZI MGUMU ZAIDI

Na Martha Mwasyeba



Kariakoo, jijini Dar es Salaam, eneo lenye pilika nyingi za wazazi na watu wengine wakinunua mahitaji ya kifamilia na binafsi, hususan kati ya mwezi Desemba na Januari, hata ikawaacha baadhi katika hali ngumu kukabili mahitaji makuu ya mwezi huu. .. **PICHA MTANDAO.**

Ni mwezi Januari mlango wa mwaka mpya. Ni kipindi chenye ushuhuda wa wazazi wengi wenye watoto wanaumiza vichwa. Huo ni mwezi unagongana na mengi kama vile kulipa kodi ya nyumba, karo za shule kwa watoto.

Hapo ndipo wazazi nao wameubatiza majina ya kila aina, ikiwamo 'mwezi mrefu usioisha' na 'mwezi mmoja ndani ya miezi mitatu' na mengine mengi.

Kupitia swali hilo gumu, ndipo gazeti la Nipashe liliamua kutafuta majibu kutoka kwa wanajamii undani wa Januari kuwa 'pasua kichwa' na gumzo kwao, kuliko miezi mingine.

Yanayomkabili mzazi yanajumuisha baadhi ya malipo kama karo za shule ambazo hata hivyo hazilipwi mara moja, kununua vifaa vya shule kama daftari, sare za shule na kwa wanaoenda bweni bajeti inatanuka.

Pia magumu mengine ya Januari ni hali ya hewa, jua kali ikiambatana na joto, bidhaa kupanda bei pamoja na ukosefu wa pesa.

**WADAU**

Mama Evance, mkazi wa Mbezi Makabe, Dar es Salaam mwenye mtoto wa darasa la sita mjini humo ana ufafanuzi: "Unajua mwezi Januari wengi wanauona ni mgumu, kwa kuwa asilimia kubwa ya wazazi wanatumia pesa vibaya mwezi Desemba kutokana na sikukuu hizi mbili Krismasi na Mwaka Mpya.'

"Wanasahau kwamba kuna jukumu kubwa la kulipa karo za watoto kwa mwezi Januari, matokeo yake inapofika wanajikuta wanahaha kutafuta pesa kwa ajili ya karo na kujikuta wanachukia mwezi Januari."

"Kwa kuwa huwa naweka mipango mapema naona mwezi Januari ni mwezi wa kawaida kama miezi mingine," anaongeza.

Mzazi wa mtoto anayesoma katika shule ya sekondari binafsi iliyoko wilaya jirani ya Bagamoyo, Mama Junior, anayeishi Mbweni, Dar es Salaam, katika mada hiyo naye ana hoja anayounganisha na maswali:

"Unajua mimi naweza kusema kuwa wazazi wengi wa kitanzania wanaishi bila mipango, maana suala la elimu na kodi za nyumba sio suala la kushtukiza kama msiba au ugonjwa, ni suala linalojulikana tangu unapoleta mtoto duniani.

"Kwanini usiwekeze pesa kidogo kidogo kwa ajili ya elimu ya wanao? Lakini cha ajabu wengi wanawekeza katika mambo yasiyo na maana, matokeo yake inapofika Januari watu 'vijasho' vinawatoka, lakini unajiuliza hivi hawa watu hawakujua kwamba mwezi Januari ni majukumu muhimu?"

Mwingine anasema asilimia kubwa ya Watanzania hawana nidhamu na utamaduni wa kutunza pesa, kwa kuzielekeza katika yasiyo ya lazima katika maisha yao.

"Anaweza kuwa na pesa aliyotunza kwa sababu ya karo au kodi ya nyumba, lakini anaposikia kuna sherehe mahali fulani au kuna nguo nzuri kaipenda anaitumia bila kufikiria kwamba hakuna sehemu yoyote atakakopata ili kurudishia ile pesa.

"Kwa kifupi maisha ya watu wengi ni ya kubahatisha na wanaishi bila nidhamu hata kidogo. Hakuna mzazi asiyejua kama anasomesha na kujua kiasi cha ada ya mwanawe au wanawe kwa mwaka," anasema.

Mwalimu Msesa kutoka Shule ya Msingi Miembe Saba, Kibaha mkoani Pwani, anachangia: "Kwanza mwezi Desemba, hasa walio kwenye sekta ya kuajiriwa wanalipwa mshahara mapema sana.

"Hivyo, pesa nyingi hutumia kwenye sikukuu na mwezi Januari ni mwezi wa kulipa karo za watoto asilimia 90, wanabana pesa kuelekeza kwenye elimu, hivyo biashara nyingi sana haziendi na kusababisha kukosa mzunguko wa pesa kwenye mfumo.

Anasema ni hali ya kawaida, watu wakilalamika sana mwezi Januari kwa kuwa na uhaba wa pesa na huwa ngumu hata kuendesha sherehe kwa kutegemea michango ya watu.

"Kwa kuwa asilimia 70 ya watu wanakuwa na uhaba wa pesa mwezi huu kwa kiwango kikubwa sana, ukitofautisha na miezi mingine ndani ya mwaka husika," anasema Mwalimu Msesa.

**MITANDAONI**

Hata kwenye mijadala ndani ya mitandao ya kijamii, mfano 'twitter' na 'WhatsApp' wazazi wengi wanajadili namna shule nyingi nchini zinagoma kupokea mtoto shuleni, pasipo kutanguliza ada kwa kiasi fulani cha makubaliano.

Ni sura ya mijadala inayoangukia pia kuthamini mahitaji ya shule kama vifaa vya kujifunzia na kodi za nyumba. Baadhi ya mijadala inapendekeza, ni vyema wazazi wanaosomesha watoto kuweka akiba katika taasisi fedha kama benki, kwani shule nyingi zina utaratibu wa kulipa karo kwa njia ya benki.

Pia katika kuepusha changamoto za kukosa karo na vifaa muhimu vya wanafunzi, kuna wazazi wanaowashauri wenzao kuweka mipango endelevu ya kuweka akiba kwa ajili ya karo na kodi za pango.

Wanasema ni mbadala chanya kuwaepusha wazazi na adha ya kukosa mahitaji kama kodi za nyumba na ada za watoto shuleni, kwani matarajio ya wamiliki wa shule na nyumba kupokea kodi na ada kwa muda mwafaka.

Ni mjadala pia unaoangukia tabia binafsi, wazazi kukumbushwa kukabiliana na majibu hasi kuhusu malipo ya madeni dhidi yao.

**SAFARI IJAYO**

Ukiwa ni mwanzoni wa mwaka mpya 2021, jamii inatakiwa kujitathmini na kuzingatia kuishi kwa malengo, ili kuondokana na dhana potofu ya kuhisi kwamba, Januari ni mwezi mgumu na unaochelewa kuisha.

Ni kanuni inayoelezwa pale inapopangwa mambo kwa uangalifu, iko bayana utafanana na miezi mingine kwa sababu 'makandokando' yake yanakuwa yamekabiliwa.

Pia mwaka 2020 unakumbukwa, janga la maradhi ya corona liliyumbisha wengi kwa mengi. Kiuchumi, akiba binafsi ziliyumba kwa kiasi kikubwa cha fedha walitumia kujikimu na familia zao.

Hapo ina maana gani? Hata wamiliki wengi wa shule wategemee wazazi wengi hawako sawa kiuchumi na si ajabu kasi ya malipo kusuasua.

Wapo waliopoteza kazi za vipato vyao, kutokana na janga hilo na wafanyabiashara wengi waliotegemea mali kutoka nje ya nchi, hawakuzipata. Yote yanaifanya Januari 2021 mwezi mgumu zaidi, kuliko nyinginezo.

Lakini, kwa sababu ni lazima maisha yaendelee, watu nao wanapaswa kujifunza nidhamu kubwa ya kutunza pesa. Ni wakati wa kubadilika.

Hivyo, mwaka 2020 umeacha darasa na nidhamu kubwa kwa wazazi na watu wengi waliozoea kuchukulia mambo yataenda kirahisi kila wakati na kama walivyopanga.

Kuna chumba cha kujifunza kwamba kuna dharura yoyote inaweza kutokea kama janga la corona lilivyopiga hodi mwaka jana.

HABARI KIMATAIFA

# Wanasheria wamwona Bobi Wine

**KAMPALA,** Uganda

HATIMAYE vikosi vya jeshi na polisi nchini Uganda, vimewaruhusu wanasheria wa aliyekuwa mgombea wa kiti cha urais, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, kumtembelea nyumbani kwake baada ya kuzuiwa ndani kwa wiki moja.

Boni Wine, alizuiwa ndani ya nyumba yake iliyopo eneo la Magere, baada ya kukamilika zoezi la uchaguzi mapema mwezi huu.

Hatua hiyo inatokana na amri iliyotolewa na mahakama kuu ya nchi hiyo juzi, baada ya Kyagulanyi na mkewe kuwasilisha ombi la kuondolewa kwa vikosi vya jeshi na polisi nyumbani kwake.

Kulingana na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), mawakili hao waliruhusiwa kumuona baada ya kukaguliwa kwenye kizuizi cha jeshi kilichowekwa karibu na nyumbani kwake.

Kwa mjibu wa mwanasheria, Asumani Basalirwa, iliwachukua muda wa saa kadhaa kuwashawishi wakuu wa Jeshi la Uganda na polisi ili kuweza kumuona mteja wao, lakini baadhi ya watu waliokwenda nao walibaki nje ya kizuizi akiwamo aliyekuwa mgombea wa kiti cha urais Jenerali Henry Tumukunde.

Basalirwa alisema walimkuta Bobi Wine akiwa na upungufu wa chakula kutokana na kuzuiwa kutototoka nje na pia wamepigwa marufuku watu kuingia nyumbani kwake ambao wangempelekea chakula. Hata hivyo hali yake kiafya sio mbaya.

"Afya yake ni nzuri, hakuna kitu chochote lakini yeye anataka kitu kimoja tu nacho ni haki yake, anataka apewe uhuru kutoka kwake nyumbani kwenda kufanya kazi yake na kurudi," alisema Asumani Basalirwa.

Mambo muhimu ambayo wanasheria hao walikwenda kujadiliana na kiongozi huyo wa chama cha (NUP) ni pamoja na kushauriana naye jinsi ya kuwasilisha kesi ya kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Januari 14, mwezi huu.

Mwanasheria alisema wanajeshi hao walidai intelijensia yao ilionyesha Bobi Wine anafanya maandilizi ya kufanya makosa, ana mipango ya kufanya vurugu na kuwaambia raia waandamane barabarani.

Madai hayo sio mara ya kwanza kwa jeshi na polisi nchini humo kuwazuia viongozi wa upinzani nyumbani baada ya uchaguzi.

**BBC**




Gari lililobeba kombora la nyuklia likipita katika maonyesho ya kijeshi. Utekelezaji wa mkataba wa kuzuia silaha za maangamizi duniani ulianza jana. **PICHA: DW**

# Watu 11 wakamatwa wizi wa watoto Ghana

**ACCRA,** Ghana

WATU 11 wamekamatwa baada ya kushukiwa kujihusisha na genge la wizi na uuzaji wa watoto nchini Ghana.

Operesheni ya kuwakamata watu hao ilifanyika juzi baada ya taarifa ya uchunguzi kubaini mtandao huo na kuwanusuru watoto wawili waliokuwa wakiuzwa kati ya dola za Marekani 5,000 na 4,800 kila mmoja.

Miongoni mwa watu waliokamatwa ni pamoja na madaktari wawili, wauguzi wanne, wanawake wawili, maofisa wawili wa huduma ya kijamii na mkunga wa kienyeji.

Ilidaiwa watu hao walikuwa wakitoa huduma katika vituo vya afya kinyume na sheria huko katika mji wa Accra na eneo jirani la Tema.

Serikali iliamini baadhi ya wanawake waliokwenda kujifungua waliarifiwa kuwa watoto wao walifariki dunia baada ya kuzaliwa.

Walisema wengine ambao hawakuweza kuangalia watoto wao wachanga, huenda walilazimishwa kuwauza.

Watoto wawili waliookolewa baada ya kuuzwa kwa waandishi waliokuwa wakichunguza taarifa hizo wamehifadhiwa katika kituo cha kuhudumia watoto cha serikali.

Mwandishi wa BBC nchini humo, alisema kuna matukio mengi ya visa ya wizi wa watoto na taarifa hiyo imewashangaza raia wengi wa Ghana kutokana na vitendo hivyo kukosa ushahidi.

Vitendo vya wizi wa watoto hivi karibuni viliripotiwa kutokea Nigeria na Kenya ambapo serikali zilichukua hatua.

**BBC**

# Dunia kutekeleza mkataba wa nyuklia

**NEWYORK,** Marekani

MKATABA wa kimataifa unaopiga marufuku silaha zote za nyuklia umeanza kutumika jana.

Hata hivyo, changamoto inayoukabili mkataba huo ni nchi zinazomiliki silaha hizo kuamua kujitenga na utekelezaji wake.

Zaidi ya theluthi mbili ya mataifa wanachama wa Umoja wa Mataifa, ziliutia saini mkataba huo mwaka 2017, ambao unaharamisha utengenezaji, umiliki wa silaha za nyuklia na kuzifanyia majaribio.

Mkataba huo unazitaka nchi wanachama kutoziruhusu nchi nyingine kuweka silaha hizo kwenye ardhi yao. Ubelgiji, Ujerumani, Italia, Uholanzi na Uturuki zina vichwa vya makombora ya nyuklia vya Marekani.

Naibu Katibu Mkuu wa shirika la wahanga wa silaha za nyuklia, Wada Masako, alimtaka Rais wa Marekani, Joe Biden, kuunga mkono juhudi hizo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alisema silaha za nyuklia ni kitisho kinachozidi kukua, na kutaka ziangamizwe haraka ili kuepusha janga kwa binadamu na mazingira ya duniani.

DW

# Marekani kuwaweka karantini wageni

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ametangaza mpango wake wa kupambana na janga la COVID-19 kwa kutia saini maagizo kadhaa ya kiutendaji yenye lengo la kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo.

Miongoni mwa masharti yanayotokana na maagizo hayo ni kuwataka wasafiri wote wanaoingia kwa ndege nchini humo kuthibitisha wamechukuliwa vipimo vya COVID-19, na kuwekwa karantini baada ya kuwasili.

Masuala mengine yaliyopewa kipaumbele na Rais Biden ni kuongeza utengenezaji wa chanjo na idadi ya vituo vya kuwapima watu, kama msingi wa kufunguliwa tena kwa shule na shughuli za biashara.

Hata hivyo, bado hakuna maelezo ya kina juu ya kilichomo katika maagizo hayo.

Rais Biden alisema utawala wa mtangulizi wake, Donald Trump, ulishindwa kupambana na janga la virusi vya corona.

DW

# Boti 'bubu' abiria, uvuvi zafichuliwa Geita

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya boti 250 katika Ziwa Victoria mkoani Geita, zikiwamo za kusafirisha abiria na uvuvi, zinatoa huduma hizo bila kusajiliwa na hivyo kukiuka kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia usafiri wa majini nchini.

Akizungumza wakati wa kampeni maalum ya elimu ya kanuni za usalama wa vyombo vya usafirishaji majini katika mialo ya Nkome, Mchangani na Makatani wilayani Geita juzi, Ofisa Mfawidhi wa Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) mkoani Geita, Rashid Katonga, aliwataka wamiliki wa boti hizo kuzisajili kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi yao.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, Mkoa wa Geita unakadiriwa kuwa na zaidi ya boti 1,000 zinazotoa huduma ya usafirishaji katika Ziwa Victoria.

Hata hivyo, alisema boti 750 zikiwamo za uvuvi pamoja na zinazosafirisha abiria na mizigo zimesajiliwa na hivyo kufanya kazi zake kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria.

"Kutosajiliwa kwa zaidi ya boti 250 kumeilazimu TASAC kutoa elimu kwa wamiliki wa boti kuhusu umuhimu wa kuthibitishwa kwa ubora wa chombo husika," alisema.

Ofisa Kitengo cha Uratibu na Uokoaji Ziwa Victoria, Joseph Mkumbo, alisema wastani wa ajali mbili hadi tatu hutokea kwenye Ziwa Victoria kila siku na kugharimu maisha ya watu.

Alisema sababu kuu ni ubovu wa vyombo vya usafiri pamoja na ubebaji wa abiria na mizigo kupita kiasi.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Emmanuel Ndomba, alibainisha mpango wa ujenzi wa vituo 10 vya kuratibu shughuli za ufuatiliaji na uokoaji katika Ziwa Victoria.



Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Omari Kigua (kushoto), akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Ramadhani Kailima, walipokutana katika viwanja vya Bunge, baada ya vikao vya Kamati za Bunge, jijini Dodoma jana. Katikati ni Mbunge wa Jimbo la Sikonge, Joseph Kakunda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC aonya mimba, VVU wachimbaji

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Dk. Severine Lalika, amewataka wananchi wanaofanya shughuli zao kwenye mialo ya uvuvi, upasuaji wa mbao, sokoni na uchimbaji wa madini, kuchukua tahadhari ili kuepuka mimba zisizotarajiwa na maradhi mbalimbali ikiwamo UKIMWI.

Alisema wataalamu wa afya Wilaya ya Ilemela wanayo ratiba ya uhamasishaji wa masuala ya afya na wanafanya mara kwa mara katika kata zote 19 zilizopo wilayani humo hasa kwenye maeneo ya mialo.

"Hizo hali zinasababisha watoto wetu wa kiume na kike hata wale ambao wapo kwenye umri wa kwenda shule, kupenda kujihusisha na shughuli za uvuvi na wakiwa huko wanakutana na adha mbalimbali kwa kuwa hawajafikia umri wa kujitambua na kujikinga kiafya," alisema Dk. Lalika.

Aliongeza kuwa watoto wengine wakiwamo wa darasa la pili, tatu na nne wanatoroka na kwenda huko kwa ajili ya kutafuta fedha na kwamba mara nyingi huishia kubakwa na wengine kupewa mimba wakiwa na umri mdogo.

Alisema sheria za nchi haziruhusu watoto kuanza kujitegemea wakiwa wadogo na kuiomba jamii kuwafichua ili serikali iwarejeshe waendelee na shule.

"Kuna kisiwa kinaitwa Bezi, Igombe na Makobe, huko ukienda kuna starehe ambazo ukiambiwa huwezi kuamini, maeneo kama hayo yana madhara kiafya," alionya Dk. Lalika.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Butuja, Kichonge Mwita, alisema katika eneo la mwalo wake, elimu inatolewa kwa sasa wakishirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya mtaa.

"Tumetoa elimu ya uzazi kwa kushirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya mtaa tumewafikia wananchi wengi na hivi karibuni tuliitisha mkutano wa hadhara ili kuwapa elimu na maelekezo, mwanzo hali ilikuwa ya hatari, lakini kwa sasa kidogo mambo yanaleta matumaini," alisema Mwita.

Aliwaomba wakazi wa mialo hiyo kuzingatia mafunzo wanayopewa ili kujenga familia njema kwa kuwa wakati mwingine mambo yanapokuwa magumu, wazazi huwakimbia watoto na kuwaacha peke yao.

## Bil. 1.3/- kupeleka maji vijijini

**Na Neema Emmanuel,** MAGU

WAKALA wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), wilayani Magu mkoani Mwanza unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 1.3 kutatua kero ya upatikanaji wa huduma ya maji katika vijijini vinne katika wilaya hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana wilayani Magu na Meneja wa RUWASA, Anna Mbawala, wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kalli kwa ajili ya kukagua miradi hiyo.

Mbawala alisema miradi hiyo inatarajiwa kukamilika na kuanza kutoa maji ili kuondoa kero ya maji katika vijiji hivyo pamoja na vingine vinavyopakana navyo.

Alisema kwa sasa wamekamilisha usambazaji wa miundombinu ya mabomba na kuanzisha vyanzo vyote vya maji na kwamba ifikapo mwezi ujao watafunga pampu na kuweka nishati ya umeme ili maji yaanze kusukumwa.

Mbawala alisema lengo la RUWASA ni kuhakikisha vijiji vyote wilayani Magu vinapata huduma ya maji kupitia miradi mbalimbali inayopangwa na serikali.

## Waziri aivaa bandari urasimu katika mizigo mafuta ya kula

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amewataka watumishi wa Bandari ya Dar es Salaam, kuondoa urasimu katika mizigo ya mafuta ya kula inayosafirishwa nje vinginevyo watafute kazi nyingine ya kufanya.

Prof. Mkenda alibainisha hayo jana jijini Dodoma, alipotembelea kiwanda cha mafuta ya alizeti cha PYXUS, kilichoko eneo la Kizota, kuangalia namna ya kuondoa uhaba wa mafuta uliopo nchini kwa sasa.

Akiwa katika kiwanda hicho, Prof. Mkenda alipokea taarifa ya mwekezaji wa kiwanda hicho, Malcom Mcgrath, kuwa wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya urasimu katika Bandari ya Dar es Salaam wanaposafirisha kontena za mafuta ghafi.

Malcom alisema hadi sasa kuna mzigo mkubwa bandarini ambao wanaendelea kuzungushwa bila kufahamu lini wataruhusiwa kuusafirisha kwenda Switzerland kwa ajili ya kutengeneza vipodozi na wateja wao wameanza kulalamika.

"Utaratibu mbovu huu, haiwezekani tukakwamishwa na mtu mmoja wakati tunahitaji wawekezaji, ninasema huyo anayewazuia ajitathmini na kuanzia sasa aanze kutafuta kazi nyingine ya kufanya na siyo katika serikali hii ya awamu ya tano," alionya.

Waziri huyo akizungumzia upungufu wa mafuta nchini, alisema hali hiyo iwaamshe wakulima na kuona ni fursa kwao katika kuzalisha kwa wingi alizeti ili walikamate soko la nje na ndani ya nchi.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 5

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Ndani ya gesti hiyo mchana huo kulikuwa na watu wengine."

"Sijui, lakini weita alihojiwa na polisi akasema hakukuwa na watu, ni mimi na Burhan tu."

"Weita hukumkuta wakati unakwenda kununua soda?"

"Sikumkuta?"

"Sasa tutaamini vipi kama kweli ulitumwa soda na kurudi ukakuta mpenzi wako ameuawa na siyo wewe ndiyo uliomuua?"

Mwajuma alibaki kanyamaza asijue la kujibu.

"Weita alikwenda wapi muda huo?"

"Sijui?"

"Je, weita anaweza kuwa ndiye muuaji wa mpenzi wako na si wewe?"

"Hapo pia afande mimi siwezi kuelewa."

"Sasa wewe unachojua ni nini?"

"Afande, hakuna hata ninachojua, ingekuwa kama kitu cha kujiandaa, ningetafuta ushahidi wa kila njia ili kujinasua kwenye hili, lakini hakuna anayejua kesho itatokea nini, ndiyo maana kila kinachozungumza hapa mimi sijui chochote. Ninachojua ni mpenzi wangu Burhan ameuawa tu tukiwa gesti na mimi ndiyo naambiwa kuwa nimemuua."

"Huoni kama ukipelekwa mahakamani kwa kesi hii adhabu yake ni kunyonywa hadi kufa au kifungo cha maisha kwa sababu ushahidi wa kimazingira unayonyesha kuwa wewe ndiye uliyetenda hilo kosa?"

Mwanaidi alianza tena kulia. "Najua afande, lakini nitafanyaje? Kila anayenihoji. Kila ushahidi unaonyesha kuwa mimi ni muuaji. Sina ujanja, namuachia Mungu tu." Akaendelea kulia safari hii kwa sauti zaidi.

Afande Jan alimsogelea, akamgusa begani. "Nyamaza. Usilie. Ni hivi Mwanaidi. Jalada hili mimi itabidi nilifuatilie vizuri zaidi. Itabidi nizame ndani kwa namna ya pekee na kwa jicho la tatu. Nina uhakika nitapata ushahidi wa kutosha hata kama ulikuwa umejificha chini ya bahari. Nakuhakikishia kama siyo wewe basi utaachiwa huru, lakini kama umefanya hivi, basi kitanzi kitakuhusu."

************************

Kilikuwa ni kikao cha muda wa siku tatu. Hoja zililetwa kwa maofisa wa polisi, lakini hatima yake kwa maslahi mapana ya Jeshi la Polisi na taifa kwa ujumla, mwafaka ulipatikana.




**Huoni kama ukipelekwa mahakamani kwa kesi hii adhabu yake ni kunyonywa hadi kufa au kifungo cha maisha kwa sababu ushahidi wa kimazingira unayonyesha kuwa wewe ndiye uliyetenda hilo kosa?**

Afande Jan John alishinda hoja yake. Pamoja na hayo dhamana ikabaki kwake yeye. Yeye alitaka mtuhumiwa aachiwe kwa dhamana. Awe nje kwa kiasi cha wiki moja hivi. Hoja zake nzito ndizo zilizofanya wakubwa zake wakubaliane naye. Na kumwamini hako kulichangiwa kutokana na kazi zake nzuri anazozifanya. Wasiwasi mkubwa ilikuwa ni juu ya kutoroka kwa mtuhumiwa Mwanaidi kwani kesi ilikuwa ni kubwa. Ni kesi ya mauaji. Jan aliwahakikisha wakubwa zake kuwa mtuhumiwa hatotoroka na dhamana yote ni juu yake.

Akiwa kwenye ofisi yake, mbele yake alikuwa amekaa Mwanaidi.

Kwa upande wake alitokea kumhusudi sana kijana yule kutokana na jinsi anavyouliza maswali yake.

Aliyaona kama ni maswali ya kutaka kujua vitu na si ya kumkandamiza.

Leo alikuwa ameitwa mbele yake. Hakuongea kitu chochote akawa amsikiliza nini ataongea.

"Mwanaidi." Aliita na kusita.

"Nimekwita hapa kukwambia jambo moja. Ni kwamba tumeamua kukuachia huru kwa muda."

"Umesema..." Mwanaidi aliuliza kama vile hajasikia.

"Nadhani umesikia Mwanaidi. Ni kwamba unakwenda nyumbani kwa muda mpaka hapo tutakapokuhitaji."

Ni jambo ambalo hakutarajia kulisikia, ingawa lilimfurahisha.

Alichotarajia ni kuambiwa kesho anapelekwa mahakamani. Hata hivyo alijua kabisa kuwa kesi haijaisha na alijua kama atatoka sababu ya juhudi kubwa ni afande mpya aliyepewa jalada lake.

Baada ya mazungumzo ya robo saa hivi. Jan alimuaga Mwanaidi ambaye alikuwa ameanza kuchangamka kwa kujua anarejea tena uswahilini.

"Kama nilivyokwambia. Hakikisha unafanya kama nilivyokwambia kila kitu kwa usahihi sawa?"

"Sawa nimesikia."

"Halafu kama nilivyokwambia usitoke au usisafiri nje ya Dar es Salaam sawa?"

Kilichofanyika hapo ni kwamba afande Jan alimsaidia Mwanaidi kila kitu, ikiwa ni pamoja na kukodi usafiri wa kumrudisha nyumbani kwao Mburahati.

**************************

Alizaliwa mkoani Singida. Tangu anasoma shule ya msingi alionekana atakuja kuwa msichana mrembo. Kila mtu alibaini kuwa mtoto huyu atakuja kuwa hazina ya uzuri.

Hata alipofika sekondari, baadhi ya wanaume wasiokuwa na staha walianza kumnyatia na kumtaka kimapenzi. Alipokuwa msichana wa haja, alishangaa kuwaona vijana na watu wazima wakimfuata na kumtaka, kitu ambacho yeye mwenyewe hakufahamu ni nini?

Mwanaidi alishindwa kuhimili. Aliwakatalia kumi, lakini akamkubalia mmoja. Huo ukawa mwanzo wa yeye kupotea.

Aliacha shule na kuanza kufuata mambo ya wanaume. Hata hivyo alichoambulia ni kuwafaidisha wanaume ambao wakishamaliza hamu zao wanamuacha kama alivyo.

Alitendwa na kutendeka. Wanaume watatu walioahidi kumuoa walimuacha na kuoa wanawake wengine. Hii ilimfanya kuanza kuchukia wanaume.

Akatoroka mkoani Singida na kwenda jijini Dar es Salaam kutafuta maisha. Akatua kwenye jiji la raha na karaha. Alikutana na kila aina ya maswahibu.

Mwendo ulikuwa ni ule ule. Wanaume waliupenda uzuri wake. Lakini wachopenda kumtumia tu na si kumuweka ndani.

Mwisho wa siku, rafiki yake mmoja akaamua kumpeleka kwenye saluni moja na kumfundisha jinsi gani ya kutengeneza nywele wanawake, pamoja na kupamba.

Haikuchukua siku nyingi akajua. Akajua kushinda aliowakuta. Akapata pesa ambazo zilimwezesha kupanga chumba kimoja Mburahati jijini Dar es Salaam.

Ndipo alipompata bwana Burhan. Kati ya wanaume wote ambao aliwahi kukutana nao ni Burhan pekee ndiye aliyeonekana kumpa pesa nyingi. Ilimfanya hata kumtumia mama yake akanunua kiwanja.

Ni Burhan pekee ndiye alionekana kumpenda na kumuahidi akimaliza shughuli iliyomleta Dar, basi angeondoka naye kwenda mkoani Mwanza ambako sasa wangekaa na kufanya utaratibu wa kufunga ndoa mbele ya safari.

Sasa ilikuwa ni ndoto iliyoyeyuka.

Alirudi tena kuwa Mwanaidi yule yule wa kusaka wanaume ambao watampa pesa ya kula tu.

Ilikuwa ni saa 10:00 jioni wakati gari ilipomshusha nyumbani kwake Mburahati akitokea Kituo Kikuu cha Polisi.

Alilakiwa na baadhi ya majirani zake na shoga zake ambao hawakudhani kama anaweza kurudi kwa sababu anachojua kuwa ni kesi isiyo na dhamana.

Labda kama mwanaume amejifia mwenyewe gesti kwa mihemko yake, presha, au kunywa dawa za kuongeza nguvu.

Lakini mwanaume ameshindiliwa visu kifuani mara nne, si rahisi kwa polisi kumuacha mwanamke aliyekuwa ndani mwanaume huyo.

"Pole shoga. Pole mwaya." Zilikuwa sauti za baadhi ya majirani na shoga zake ambao walishtukia tu anashuka kwenye gari.

"Ahsanteni sana." Aliwajibu, lakini akionekana hapendi sana kulizungumzia suala hilo.

"Naomba niacheni shoga zangu. Nimekaa mwezi mmoja na nusu nalala usingizi wa mang'amung'amu. Halafu halijaisha ni kwamba niko nje tu kwa dhamana." Aliwasihi shoga zake watoke nje wamuache apumzike.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# BAYERN WAMFUNGIA KAZI UPAMECANO




**MUNICH,** Ujerumani

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema klabu hiyo inamkodolea macho, Dayot Upamecano, hata kama ni mapema mno kutarajia mlinzi huyo wa RB Leipzig kujiunga nao.

Upamecano mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akitajwa kama mmoja wa walinzi bora wa kati Ulaya katika misimu ya hivi karibuni na imedokezwa anaweza kujiunga na timu kubwa mwishoni wa msimu.

Bayern imekuwa ikihusishwa sana na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, hasa kutokana na ukweli kwamba, David Alaba anatarajia kuondoka kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu.

Rummenigge amethibitisha mipango ya kutaka kumsajili nyota huyo, lakini hakuna ofa yoyote waliyoiandaa hadi sasa.

Aliliambia gazeti la Bild kwamba, Upamecano atakuwa "pale Leipzig angalau hadi mwishoni mwa msimu", akiongeza kuwa itakuwa "mapema sana" kujiridhisha kwamba atajiunga na mabingwa hao.

"Tunafuatilia hili bila shaka yoyote, sio yeye tu, lakini kutokana na nafasi na wapi ambapo tunatakiwa kufanya marekebisho," alisema.

Bayern pia inaweza kumpoteza Jerome Boateng mwishoni mwa msimu huu, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 wake unamalizika Juni, mwaka huu.

# Rooney: Pogba amebeba mafanikio ya United EPL

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba anaweza kutengeneza tofauti kwa Manchester United na kuwasaidia kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu, kwa mujibu wa gwiji wa klabu hiyo, Wayne Rooney.

Kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer kiliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Fulham Jumatano, matokeo ambayo yaliwafanya warudi kileleni mwa msimamo wa ligi.

Wakati Manchester City na Leicester City wakiwa wamepitwa pointi mbili na bingwa mtetezi, Liverpool amepitwa pointi sita wakiwa na mchezo mmoja mkononi, Rooney anahisi kikosi chake hicho kinaweza kubeba taji msimu huu.

Mfungaji huyo wa wakati wote wa United, amewataja pia, Bruno Fernandes na Edinson Cavani watakisaidia kikosi hicho kushinda, ingawa Rooney anahisi Pogba ndio ameshikilia funguo ya mafanikio.

"Miaka michache iliyopita United haikuwa na uwezo wa kuwa kwenye mbio za kuwania ubingwa," alisema Rooney, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa Derby County, akiwaambia waandishi wa habari.

"Ninachofikiri kwa sasa, wamejenga kikosi cha wachezaji. Ujio wa Fernandes umesaidia kwa kiasi kikubwa.





# *Koeman akasirika Barca kukosa penalti*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman alikasirishwa na kikosi chake kukosa penalti mbili wakati wakiibuka na ushindi kwenye mchezo wao wa Copa del Rey dhidi ya Cornella.

Miamba hao wa Katalunya walihitaji hadi muda wa ziada baada ya mabao ya Ousmane Dembele na Martin Braithwaite kuwafanya watoka dimbani kwa ushindi wa 2-0, juzi Alhamisi.

Golikipa wa Cornella, Ramon Juan alikuwa kikwazo kwa Barca, akiokoa michomo saba, huku mbili zikiwa ni penalti kutoka kwa Miralem Pjanic kipindi cha kwanza na Dembele kipindi cha pili.

Kukosa kwa nafasi hizo mbili muhimu kuliwafanya Barca kwenda hadi muda wa ziada ili kupata ushindi huo.

Barca sasa imekosa penalti tano kati ya nane katika mashindano yote, na Koeman alikuja juu kulaumu hali hiyo.

# Mshahara wa Eriksen waikimbiza Leicester

**LONDON,** England


KLABU ya Leicester City wameamua kuachana na mpango wao wa kutaka kumsajili kwa mkopo, Christian Eriksen kutoka Inter Milan, kwa sababu ya mshahara wake mkubwa.

Kwa mujibu wa gazeti la Telegraph, mabingwa hao wa zamani wa Ligi Kuu England walijaribu kufanya makubaliano ya kunasa saini ya Eriksen.

Hata hivyo, mara tu walipogundua mshahara wake unafikia takriban pauni 300,000 kwa wiki, na Inter haikutaka kugharamia zaidi, Leicester wamesogea kando kwenye dili hilo.

Kiungo huyo wa Denmark amehusishwa na kurejea kwenye Ligi Kuu England, huku pia Tottenham Hotspur, ambako aliondoka mwaka mmoja uliopita kwa zaidi ya euro milioni 20, ikitajwa pia kutaka kumrudisha.

Inter wangependa kumuuza, lakini bado hawajapata klabu ambayo iko tayari kulipa bei inayotajwa.





# ZIDANE AKALIA 'KUTI KAVU' MADRID

**MADRID,** Hispania

MAJALIWA ya Zinedine Zidane pale Real Madrid yameibua maswali, kwa mujibu wa gazeti la AS.

Madrid walitupwa nje na timu ya Daraja la Tatu ya Alcoyano kwenye michuano ya Copa del Rey Jumatano, na hivyo kuibua maswali kuhusu hatima ya Zidane.

Zidane amekalia kuti kavu na kwa mujibu wa habari kutoka ndani ya Real Madrid zilizonaswa na gazeti la AS, Mfaransa huyo anaweza kutimuliwa.

Hata hivyo, ripoti hiyo inasema wanasubiri hadi kuanza tena kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo itaendelea mwezi ujao.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid, Raul ndiye anayetajwa kuwa kwenye nafasi ya kuchukua nafasi yake.

Madrid ipo katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakipitwa pointi saba na Atletico Madrid waliopo kileleni, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

# *Marseille wamsajili Milik*

**PARIS,** Ufaransa

STRAIKA Arkadiusz Milik amejiunga na timu ya Marseille kwa mkopo akitokea klabu ya Napoli hadi mwaka 2022 na anaweza kupewa mkataba wa kudumu wa euro milioni 12.

Milik mwenye umri wa miaka 26, anaelekea klabu ya Ligue 1 baada ya misimu minne na nusu huko Napoli, ingawa hajacheza kabisa msimu huu 2020-21, baada ya kukataa kuongeza mkataba.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland alifunga mabao 48 katika michezo 122 katika Serie A, baada ya kuwasili kutoka Ajax kwa kitita cha euro milioni 35 mwaka 2016.

Majeraha ya magoti yalimkwamisha katika klabu ya Napoli, na uhamisho wake kwenda Marseille ulithibitishwa jana Ijumaa.


Wakati Napoli walisema Marseille walikuwa na "wajibu wa kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu", upande huo wa Ligue 1 ulidai kuwa ilikuwa chaguo.

Milik pia alikuwa akihusishwa na timu za Ligi Kuu England, Tottenham Hotspur na Everton, lakini alifurahi kupata uhamisho wa Marseille, ambao wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligue 1 - alama 10 nyuma ya Paris Saint-Germain.

"Nina furaha na fahari kutangaza kwamba mimi ni mchezaji rasmi wa Olimpikique de Marseille, moja ya klabu maarufu hapa Ulaya," Milik aliandika kwenye Twitter.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: NILAUMIWE MIMI KWA KICHAPO

●●● Ni baada ya kupoteza mechi dhidi ya Burnley licha ya kutawala mchezo huo kwa...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amesema kipigo cha Liverpool kutoka kwa Burnley ilikuwa ni "ngumi ya uso", lakini amekubali yeye ndio wa kulaumiwa baada ya kichapo hicho cha bao 1-0 katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield juzi usiku.

**Liverpool ambayo ni bingwa mtetezi wa Ligi Kuu England, kwa sasa wanapitia kipindi kigumu, hawajaonja ladha ya ushindi tangu ilipotoka sare ya bila kufungana dhidi ya Manchester United.**

Ilimaliza mchezo ikiwa na umiliki wa mpira asilimia 72 na ilipiga jumla ya mashuti 27 yaliyolenga lango yalikuwa sita, huku wapinzani wao wakipiga jumla ya mashuti sita na manne yalilenga lango.

Lakini bahati haikuwa kwao, kwani wakajikuta wakifungwa bao hilo kwa mkwaju wa penalti likifungwa na Ashley Barnes dakika ya 83.

Burnley wamevunja rekodi ya Liverpool ya kucheza mechi 68 bila kufungwa, ambapo mara ya mwisho kufungwa ilikuwa ni Aprili, mwaka 2017.

Kichapo hicho kinaifanya Liverpool ibaki na pointi zake 34 ikiwa nafasi ya nne, huku Burney ikiwa nafasi ya 16 na pointi 19 na kinara ni Manchester United ambayo imekusanya jumla ya pointi 40.

"Mimi ndio ninapaswa kulaumiwa, kwani vijana walicheza kwa bidii kubwa, lakini hawakupata ushindi," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumepoteza mchezo, nadhani ilikuwa ni jambo gumu ambalo lilikuwa haliwezekani, lakini imetokea ninapaswa kulaumiwa mimi kwa kuwa vijana walipambana kutimiza majukumu yao ila bahati haikuwa kwao," aliongeza.

"Tulikuwa na mpira asilimia kubwa na tulitengeneza nafasi nyingi, lakini hatukuzitumia, hivyo kwa hali hii ni sawa maamuzi ambayo ninaweza kufanya yanaweza kuwa magumu, lakini hakuna chaguo kwa kuwa hali imeshatokea na haiwezekani kubadilika.

"Nilisema kwenye mchezo wetu uliopita kuna jambo ambalo halifanyi kazi ila ni lazima tufanye kazi kwa uharaka na kurejea kwenye ubora wetu," alisema.

## ZISIKUPITE

### LEICESTER YAMTOSA ERIKSEN

LEICESTER City imeachana na mpango wao wa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark anataka mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki. ***(Telegraph)***

### UPAMECANO SOKONI

BAYERN wamethibitisha haja yao ya kutaka kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, ambaye katika mkataba wake ana kipengele cha kumwacha kwa pauni milioni 40. ***(Mirror)***

### MAN UNITED, CITY VITANI

MANCHESTER United, Manchester City na Chelsea kwa pamoja wameonyesha nia yao katika ya kumtaka beki, Dayot Upamecano ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### ODEGAARD ANUKIA ARSENAL

LICHA ya klabu mbalimbali kuonyesha nia ya kumtaka kiungo wa kati wa Real Madrid, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, anakaribia kukamilisha uhamisho wake wa mkopo kuelekea Arsenal. ***(Sport - in Spanish)***

### MC CARTHY ANUKIA CELTIC

KIUNGO wa kati wa Crystal Palace, James McCarthy mwenye umri wa miaka 30, analengwa na klabu ya Celtic ya nchini Scotland. ***(Mail)***

### RICE KUSHUSHWA BEI

WEST Ham huenda wakashusha bei ya kiungo wa kati, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, hadi kufikia pauni milioni 50, kwa sababu ya athari za janga la virusi vya corona. ***(90min)***

### DELE AITAMANI PSG

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, amemwomba mwenyekiti, Daniel Levy asimwekee pingamizi katika uwezekano wake wa kuhamia Paris St-Germain. ***(90min)***

### KING APANDIWA BEI

WEST Ham wanajiandaa kuongeza dau lao la pauni milioni 16 ili kumsajili mshambuliaji Bournemouth, Joshua King mwenye umri wa miaka 29 ambaye ni raia wa Norway. ***(Sun)***

### CAICEDO KUTUA BRIGHTON

KIUNGO wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 19, jana Ijumaa alitarajiwa kusafiri kuelekea England kukamilisha mkataba wa pauni milioni 4.5 wa kuhamia Brighton kutoka klabu ya Independiente del Valle. ***(Sky Sports)***

### VILLAS-BOAS ASHANGAA

KOCHA wa Marseille, Andre Villas-Boas amesema ofa kwa kiungo wa kati wa Aston Villa, Morgan Sanson mwenye umri wa miaka 26, "inasikitisha". ***(Mail)***

## Mtibwa Sugar yasaka pointi 21

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha timu yake inakuwa mahali salama, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, amesema anahitaji kupata ushindi katika mechi zake saba za nyumbani zilizobakia kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema timu yake imebakiza michezo 17, na anahitaji kukusanya pointi 21 katika mechi zote saba atakazocheza nyumbani ili kujihakikishia anakaa katika mazingira mazuri.

Hitimana alisema anahitaji pia kutafuta pointi nyingine muhimu katika michezo 10 ya ugenini ikiwamo minne ya mwisho ambayo atacheza ugenini.

"Tupo katika nafasi mbaya, nimeongea na uongozi pamoja na wachezaji wangu kuhakikisha tunafikia malengo yetu katika hizi mechi 17, nina imani itakuwa ngumu ila wakiamua tunaweza kufanya vizuri."

Kocha huyo alisema anataka kuona mapambano yake yanafanikiwa na kukwepa kushuka daraja moja kwa moja au kuwa miongoni mwa timu zitakazocheza mechi za mtoano.

"Sihitaji kufika huko, nimeshawaeleza viongozi wangu kuhusu mkakati huo, mbali na kutofanya usajili kipindi cha dirisha dogo, lakini nina imani wachezaji tulikuwa nao tutawajenga kisaikolojia na kuwapa mbinu za kumaliza katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo," alisema Hitimana.

## Wachezaji Biashara waingia matatizoni

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, ametaka wachezaji wake 15 ambao ni Watanzania kukatwa sehemu ya mishahara yao kutokana na kosa la kuchelewa kurejea kwenye kikosi hicho kwa wakati.

Baraza aliliambia gazeti hili amechukua uamuzi huo kwa sababu hajafurahishwa na kitendo hicho cha utovu wa nidhamu ambacho kinarudisha nyuma mipango yake ya kuijenga timu.

Kocha huyo alisema adhabu watakayopata itakuwa ni fundisho kwa wachezaji wengine na anaamini itasaidia kurejesha nidhamu katika timu.

"Jambo la kushangaza wachezaji wa kigeni wote waliwasili kwa wakati mwafaka na baadhi ya nyota wengine, lakini nyota 15 ambao wako katika mipango yangu ya kikosi cha kwanza wananiangusha na watatumikia adhabu hiyo."

Aliongeza baadhi ya timu zimekuwa na matokeo mabaya kwa sababu wachezaji wake wameweka nidhamu pembeni jambo ambalo linawakwamisha kupata maendeleo.

# MKUTANO MKUU ZFF KUFANYIKA LEO UNGUJA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUTANO Mkuu wa mwaka wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), unatarajiwa kufanyika leo Kisiwani Unguja, imeelezwa.

**Awali mkutano huo ulipangwa kufanyika Januari 9, mwaka huu, lakini ulisogezwa mbele kutokana na sababu mbalimbali.**

Mkutano huo utakuwa ni wa kwanza kufanyika tangu uongozi uliopo madarakani kuchaguliwa na kutoka kilichoitwa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) na sasa kuwa shirikisho yaani ZFF.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Katibu Mkuu wa ZFF, Haji Hassan 'Kibabu', alisema maandalizi ya kuelekea katika mkutano huo yamekamilika na wajumbe wote kutoka Kisiwani Pemba wamethibitisha kuwasili kwa ajili ya kuhudhuria kikao hicho.

Kibabu alisema mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wa shirikisho hilo ambao tayari walishapewa taarifa ya kuwapo kwa mkutano huo ambao utafanyika kwenye ukumbi wa Chuo cha Mafunzo, Unguja.

Kiongozi huyo alisema mkutano huo ndio utakaotoa mwongozo wa maendeleo na mustakabali wa soka la Zanzibar kwa kupokea michango yenye tija kutoka kwa wanachama wa ZFF.

Alimtaja mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana.

Wakati huo huo, Kibabu alisema wanatarajia kuwa na mafunzo ya uongozi kwa wenyeviti wa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar na Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo yataendeshwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Alisema mafunzo hayo kwa viongozi wa timu za Ligi Kuu Zanzibar yatakayofanyika Januari 23, mwaka huu na siku inayofuata itakuwa ni kwa wenyeviti wa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara.




Mshambuliaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), John Bocco (kushoto), akijifua kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya pili ya Kundi D ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Namibia itakayochezwa leo katika Mji wa Limbe nchini Cameroon. Kulia ni beki wa timu hiyo, Ibrahim Ame. **PICHA: TFF**

## *Kova ashikilia hatima ya Mkude*

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Nidhamu ya Simba iliyoko chini ya Mwenyekiti, Suleiman Kova, inatarajia kukutana na kiungo wa timu hiyo, Jonas Mkude ambaye alikuwa amesimamishwa na mabosi wake kutokana na kosa la utovu wa nidhamu.

Kikao hicho kinafanyika ikiwa ni siku mbili baada ya kiungo huyo kuomba radhi kwa viongozi, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kwa kosa alilofanya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, alisema Kamati ya Nidhamu imepanga kukutana na Mkude kwa ajili ya mahojiano rasmi na baada ya hapo itafahamika hatima yake.

Gonzalez alisema bado Mkude ni mchezaji halali wa Simba na baada ya kumuhoji na kuwasilisha utetezi wake katika Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, watatangaza rasmi hatua itakayochukuliwa.

Alisema bodi imeahidi kuufanyika kazi utetezi wa nyota huyo na kuongeza kwa sasa wanahitaji kuona wachezaji wa klabu hiyo wanakuwa na nidhamu.

"Jambo la Mkude litakwisha baada ya kesho (leo), kamati ya nidhamu itakapokutana naye na kuleta kwetu maelezo, pia suala la Bernard Morrison naye bado ni mchezaji halali wa Simba, alikuwa mgonjwa, amepona na Jumapili ataingia kikosini," alisema kiongozi huyo.

# Michezo

Jumamosi Januari 23, 2021

Nipashe





## Klopp: Nilaumiwe mimi kwa kichapo

UKURASA 22




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez (kushoto), akizungumza kuhusu mashindano mapya ya kimataifa yatakayojulikana kwa jina la Simba Super Cup yatakayofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Stars, Namibia mechi ya kisasi

**Na Adam Fungamwango**

MACHO na masikio ya Watanzania yanatarajia kuelekezwa nchini Cameroon wakati Timu ya Taifa (Taifa Stars), itakapotupa karata yake ya pili dhidi ya Namibia katika mechi ya Kundi D ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itakayochezwa leo Mjini Limbe.

Taifa Stars ambayo itashuka dimbani kuanzia saa 4:00 kwa saa za Afrika Mashariki, inahitaji ushindi tu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoendelea nchini humo.

Kikosi hicho cha Stars kinachofundishwa na Etienne Ndayiragije kitashuka uwanjani kikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 2-0 na Zambia wakati Namibia yenyewe ilibugizwa magoli 3-0 na Guinea katika mechi zao za kwanza.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola, alisema jana anaamini watafanya vyema katika mechi hiyo, baada ya kufanyia kazi upungufu yaliojitokea kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Zambia.

"Hayakuwa makosa makubwa sana, yalikuwa ya kimchezo tu, kama vile ile penalti ya Kapombe (Shomary), mpira ulimgonga kwa bahati mbaya na mwamuzi aliamua hivyo, " alisema Matola.

Nahodha wa kikosi hicho, Kapombe alisema walifungwa mechi ya kwanza kutokana na kupungua kwa umakini katika kipindi cha pili tofauti na walivyocheza vizuri dakika 45 za kwanza za mchezo huo.

"Tunachotakiwa kukifanya ni kucheza kwa umakini mkubwa vipindi vyote viwili kutokana na umuhimu wa mchezo wenyewe. Yale tumeyaacha, tunaangalia mechi hii sasa," alisema Kapombe.

# Simba, Mazembe kupimana

### ●●● Wapo pia Al Hilal kutoka Sudan, ni katika michuano ya Simba Super Cup, ikilenga...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba watakaribisha TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), katika mechi ya mashindano maalumu ya Simba Super Cup itakayochezwa Januari 31, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

**Mashindano hayo yatakayochezwa kwa mara ya kwanza yatashirikisha timu tatu ambazo ni pamoja na wenyeji Simba, TP Mazembe na Al Hilal kutoka Sudan.**

Akizungumza jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema mashindano yameandaliwa kuzipa maandalizi timu hizo zilizotinga hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Gonzalez alisema mechi ya ufunguzi itachezwa Januari 27, mwaka huu, kati ya Simba dhidi ya Al Hilal na michezo yote itapigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

"Hii michuano itatusaidia kuimarisha kikosi chetu kuelekea maandalizi ya Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini tunahitaji kufanya vizuri katika mashindano hayo mafupi na ikiwezekana kubakiza kombe letu." alisema Gonzalez.

Kiongozi huyo alisema pia kikosi cha Simba kitaingia kambini kesho kikiwa chini ya makocha wasaidizi ambao watatambulishwa wakati wowote kuanzia leo pamoja na Kocha Mkuu ambaye atatangazwa siku zijazo.

"Kabla ya mashindano kuanza tutakuwa tumeshamtangaza kocha mpya, hivyo kesho (leo), mashabiki watamjua kocha mpya wa Simba wasiwe na mashaka. Kikubwa ni kwamba tupo imara na hatuna mashaka yoyote mashabiki wasiwe na mashaka kila kitu kitakwenda sawa," aliongeza Gonzalez.

Alisema watatumia mashindano hayo pia kutambulisha wachezaji wapya ambayo wamesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo ambalo lilifungwa rasmi Januari 15, mwaka huu.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema malengo makubwa waliyonayo ni kupata kocha ambaye ataisaidia timu yao kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara pamoja na kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Manara alisema Simba inahitaji kufanya vizuri zaidi hivyo inatakiwa kuajiri kocha ambaye anauzoefu na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo wanashiriki kwa sasa.

Alisema michuano hiyo itawasaidia kuongeza nguvu katika mbio za ubingwa pamoja na kushinda mechi zao za 'viporo' za Ligi Kuu Tanzania Bara watakazocheza mapema mwezi ujao.

Kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wawakilishi hao wa Tanzania Bara wamepangwa katika Kundi A pamoja na Al Ahly ya Misri na AS Vita ya Kinshasa DRC.

Simba itaanzia ugenini dhidi ya AS Vita ifikapo Februari 13, mwaka huu, halafu siku 10 baadaye itawakaribisha Al Ahly kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >